


KIMATAIFA
Uk. 19
## Israel yapiga maeneo 400 Gaza



UCHUMI
Uk. 15
## Tufanye haya "tunapojitafuta" kuachana na mkaa na kuni



KOLAMU
Uk. 11
## Uzushi umepata majibu ya kisayansi Bandari

Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo




| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00035 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Oktoba 25 - 31, 2023 |

# Rais Dk. Samia akoleza ushirikiano Tz, Zambia

Uk. 4



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akiweka shada la maua kwenye mnara wa kumbukumbu ya Wapigania Uhuru (Mashujaa) jijini Lusaka, Zambia katika maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa nchi hiyo jijini Lusaka jana. Picha: (Ikulu)

## ... Atamani mradi wa umeme (JNHPP) uanze mapema

Uk. 2

## Watatu familia moja wafariki

Uk. 2



Uk. 3

## 'Walinzi MOI boresheni huduma kwa wateja'

## Mil. 1.6 kufanya mtihani darasa la 4

Uk. 4



## Wakunwa uteuzi wa Makonda

Uk. 5



# Watatu familia moja wafariki ajali ya gari

**Na Mwandishi Wetu**

WATU watatu wa familia moja, wamefariki dunia baada ya magari mawili kugongana uso kwa uso katika Kijiji cha Mbala Kata ya Vigwaza Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani.

Ajali hiyo ilitokea juzi saa 3:00 usiku kwa kuhusisha gari dogo aina ya Kluger yenye namba za usajili T.478 DCQ ikitokea Iringa kwenda Dar es Salam likiwa na watu saba wa familia moja lililogongana na gari lenye namba T.851 AQC aina ya Scania iliyokuwa ikitokea Dar es Salam kwenda Morogoro.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, alisema katika ajali hiyo watu wanne walijeruhiwa akiwemo Amina Kondo (77), Abdallah Ally (mwaka mmoja) wakazi wa Manzese jijini Dar es Salam na wanaume wengine wawili ambao hawajafahamika majina yao.

Kamanda Lutumo alisema majeruhi na waliofariki dunia, wote walikuwa katika gari ndogo iliyokuwa ikitokea Iringa kwenda Dar es Salam ambayo ilikuwa imepakia ndugu wa familia moja.

Alieleza kwamba chanzo cha ajali hiyo ni gari ndogo kutaka kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari na hivyo kugongana uso kwa uso na lori hilo.

**Kamanda Lutumo alisema majeruhi na waliofariki dunia, wote walikuwa katika gari ndogo iliyokuwa ikitokea Iringa kwenda Dar es**

# Haja kubwa kutumika kubaini Kifua Kikuu

**Na Godfrey Sanga**

WIZARA ya Afya kupitia Mpango wa Kutokomeza Kifua Kikuu (TB), wameongeza kipimo kingine cha ugunduzi wa ugonjwa huo kwa kutumia haja kubwa.

Kipimo hicho ni kwa watu wa makundi maalum wakiwemo watoto chini ya miaka mitano ambao hawana uwezo wa kutoa sampuli ya makohozi, wagonjwa wanaoishi na maambukizi ya Virus vya Ukimwi na wagonjwa waliolala kitandani kwa muda mrefu kutokana na kuzidiwa.

Kwa mujibku wa taarifa iliyolewa jana na mtandao wa kijamii wa Instagram wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Temeke (TRRH), hospitali hiyo ilianza kutoa huduma za kiuchunguzi kwa wahisiwa wa kifua kikuu kupitia kipimo hicho kipya ambacho kinatumia vinasaba na kufanikiwa kugundua wagonjwa kadhaa ikiwemo mtoto wa miezi mitano.

Dk. Rose Chagama, mtaalamu wa Kifua Kikuu na Ukoma kutoka hospitali hiyo, alieleza kuwa kipimo hicho ni kipya kwa Tanzania na kwa Hospitali ya Temeke na kkwamba huduma hiyo ilianza kutolewa mwishoni mwa Septemba, mwaka huu.

Dk. Chagama alisema kipimo cha Kifua Kikuu kupitia haja kubwa, ni kipimo mahususi kwa makundi hayo maalum yaliyotajwa.

Aidha, kupitia kipimo hicho, alisema itasaidia kuongeza ufanisi wa utoaji huduma na kupunguza vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano na kwa wagonjwa waishio na maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwani Kifua Kikuu ni moja ya magonjwa nyemelezi yanayowapata na wengi kupoteza maisha.

Wizara ya Afya inatajwa kuendelea kuboresha afya za wananchi kwa kuweka mazingira wezeshi ya kufanya tafiti mbalimbali zinazosaidia ugunduzi wa njia mbadala za kuimarisha afya na kupunguza vifo nchini.

**Dk. Chagama alisema kipimo cha Kifua Kikuu kupitia haja kubwa, ni kipimo mahususi...**

## KWA UFUPI:



## Samia atamani mradi JNHPP uanze mapema

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, anatamani mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), uanze mapema ili Watanzania wapate umeme wa uhakika.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko alipokutana na kufanya kikao na ujumbe wa Waziri wa Nyumba, Nishati na Maendeleo ya Makazi kutoka nchini Misri, Dk. Assem Elgazzar kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa JNHPP jijini Dar es Salaam.

Dk. Biteko alisema Rais Dk. Samia ana mategemeo makubwa kuhusu kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo na anatamani mwanzoni mwa mwaka 2024 utekelezaji wake uanze na kuongeza kuwa mradi wa JNHPP ndiyo mwarobaini wa kutatua changamoto ya hali ya upatikanaji wa umeme nchini.

## Mikakati kuinua vijana kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu, Dar**



SERIKALI imeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha inainua ustawi wa vijana kiuchumi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba wakati wa maadhimisho ya Siku ya Umoja wa Mataifa katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam.

Waziri Kairuki alisema njia mbalimbali zimekuwa zikitumika na serikali katika kuhakikisha kwamba vijana wanapiga hatua kiuchumi.

"Kwa upande wa Tanzania Bara, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 inafanyiwa mapitio ili kuakisi hali ya sasa ya maendeleo ya vijana, vipaumbele na changamoto," alisema.

# `Wataalamu sekta ya afya wasaidiwe ujuzi'

**Kabla ya mtaalam kutoka hospitali za pembezoni kumpa rufaa mtoto kwenda kwenye hospitali ya juu, inabidi...**

**Na Mwandishi Wetu MNH**

WATAALAM wa sekta afya wanahitaji msaada wa ujuzi na maarifa kuliko aina nyingine ya misaada kwa kuwa itasaidia kusambaza maarifa hayo kwa vizazi na vizazi na hatimaye kusaidia kuokoa maisha.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Profesa Mohamed Janabi, wakati akifungua mafunzo maalumu ya siku tano ya wataalamu wa upasuaji kwa watoto jijini Dar es Salaam jana yanayohusisha washiriki kutoka hospitali zilizo mikoa ya pembezoni mwa Tanzania, ambayo yanatolewa na wakufunzi kutoka Oxford University kwa ufadhili wa shirika la Kids-OR.

"Kabla ya mtaalam kutoka hospitali za pembezoni kumpa rufaa mtoto kwenda kwenye hospitali ya juu, inabidi ahakikishe kuwa amempa huduma nzuri za awali ili kuokoa maisha na kumsaidia afike salama hii inawezekana tu ikiwa mtaalam husika atakuwa na maarifa ya kutosha" Alisema Janabi.



# Milioni 710/- kuimarisha huduma za afya Mbinga

**Niwapongeze sana wananchi wa Kata ya Muungano kwa kuIunga mkono Serikali ya Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuleta maendeleo ili kuhakikisha afya zenu na Watanzania kwa jumla, zinakuwa salama.**



**Na Mwandishi Wetu, Mbinga**

SERIKALI kupitia Wizara ya Afya imesema kuwa Kituo cha Afya Kindimbachini kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma, kitapokea vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 710 ndani ya mwezi mmoja ili kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma za afya kituoni hapo.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, wakati wa uzinduzi wa Kituo cha Afya Kindimbachini kilichopo katika Kata ya Muungano jana.

Dk. Mollel alisema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini kwa kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya vinakuwa na miundombinu bora, vifaa tiba na vitendanishi, dawa pamoja na uwepo wa wataalamu wa afya.

Aidha, aliwapongeza wananchi wa kata hiyo kwa kuchangia Sh. milioni 22 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya pamoja na Sh. milioni tisa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya.

"Niwapongeze sana wananchi wa Kata ya Muungano kwa kuIunga mkono Serikali ya Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuleta maendeleo ili kuhakikisha afya zenu na Watanzania kwa jumla, zinakuwa salama," alisema Dk. Mollel.

Pia alitoa wito kwa wananchi hao kuendelea kushirikiana na serikali yao katika kuleta maendeleo nchini ili kuweka mazingira rafiki kwa vizazi vya baadaye.

Awali, Diwani wa Kata ya Muungano, Paulo Kayombo, aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi.

Kayombo alisema kabla ya hapo, wananchi walilazimika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya katika vituo vingine hususani wajawazito wakati wa kujifungua.

# 'Walinzi MOI boresheni huduma kwa wateja'

**Na Mwandishi Wetu-MOI**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo (MOI) Prof. amefanya kikao cha kimkakati na, viongozi wa SUMA JKT Makao makuu na walinzi wa taasisi hiyo kwa lengo la kujadili changamoto mbalimbali na kuzitafutia ufumbuzi ili kuboresha huduma kwa wateja.

Katika kikao hicho kilichofanyika jana ukumbi wa MOI mpya Prof. Makubi aliwaomba walinzi hao (SUMA JKT) kuwa wavumilivu katika kuwahudumia wagonjwa na ndugu wa wagonjwa ili kuepusha migogoro baina yao kwa sababu eneo la Hospitali linahitaji upendo, huruma na majitoleo.

Pia Mkurugenzi huyo alitoa rai kwa ndugu wa wagonjwa wanaofika MOI kusindikiza au kuwajulia hali wagonjwa kuheshimu miongozo, taratibu na muda wa kuwaona wagonjwa waliolazwa wodini.

"Muda wa kuona wagonjwa ni saa 12 :00 asubuhi hadi saa 1:00 asubuhi, muda wa kuleta chakula ni kuanzia saa 6:30 mchana hadi saa 8: 00 mchana na kuona wagonjwa ni kuanzia saa 10:00 jioni hadi 12:00 jioni na idadi ya watu wanaotakiwa kuingia wodini kumuona mgonjwa ni wawili kwa kupokezana kila baada ya dk 15, tuzingatie hilo" amesema Prof. Makubi. Aidha, walinzi pia wapo kwa ajili ya usalama wa kila mmoja pamoja wa wagonjwa , ndugu zao na mali zao.

Aidha amesema menejimenti inatafakari ombi la wananchi la kutaka kuongezwa kwa idadi ya ndugu wa wagonjwa waliolazwa wanaoruhusiwa kumuona mgonjwa bila kuathiri usalama, afya za wagonjwa na ndugu zao.



# Chakuhawata Kongwa chapata uongozi upya

**Na Mwandishi Wetu, Kongwa**

CHAMA cha Kulinda na Kutetea Haki za Walimu Tanzania (Chakuhawata) Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, kimekamilisha safu ya uongozi ngazi ya wilaya.

Lengo la uchaguzi huo uliofanyika katika mji mdogo wa Kibaigwa wilayani humu mwishoni mwa wiki, lilikuwa ni kukamilisha safu ya uongozi ngazi ya wilaya kutokana na waliokuwepo kukaimu nafasi hizo.

Awali, Msimamizi Mkuu wa uchaguzi huo, Mwalimu Abdulazizi Lubuva ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chakuhawata Wilaya ya Chamwino, aliwasomea wajumbe kanuni muhimu zinazoongoza uchaguzi na kuwasisitiza wazizingatie.

Nafasi za uongozi zilizotakiwa kujazwa ni za viongozi wa matawi kutoka shule mbalimbali zinazounda kata ambao ni Mwenyekiti, Katibu, Mweka Hazina ngazi ya Tawi na Mwakilishi wa Wanawake katika ngazi hiyo.

**Najua imani kubwa mlinayo nayo kwetu, nawahakikishia tutakuwa viongozi watumishi kwenu kuhakikisha walimu wanapata haki zao kwa wakati.**

Mwakilishi wa Tawi kwenye vikao vya wilaya, alichaguliwa Mwalimu Kazema Kazema, kuwa Mwenyekiti wa Wilaya na Mwalimu Onesmo Nakomolwa, akishindwa nafasi ya Katibu wa Wilaya. Nafasi ya Mwekahazina wa Wilaya, ilikwenda kwa Mwalimu Mikidadi Irumba na Mwalimu Fredrick Bakuza alichaguliwa kuwa Mwakilishi wa Wilaya kwenye Mkutano Mkuu Taifa.

Kadhalika, Mwalimu Suzana Mtata, aliibuka kidedea katika nafasi ya Mwakilishi wa Kitengo cha Wanawake Wilaya na nafasi ya Mwakilishi wa Walimu wenye Mahitaji Maalum, ikienda kwa Mwalimu Veronica Sulle.

Mwalimu Kazema ambaye ni Mwenyekiti Mteule, aliwahakikishia wajumbe kusimama thabiti kutetea haki na stahili mbalimbali za walimu, lakini pia akisisitiza wajumbe kutimiza wajibu wao wa kufundisha kikamilifu katika vituo vyao vya kazi.

Naye Katibu Mteule Mwalimu Onesmo alisema: "Najua imani kubwa mlinayo nayo kwetu, nawahakikishia tutakuwa viongozi watumishi kwenu kuhakikisha walimu wanapata haki zao kwa wakati."

# Rais Dk. Samia akoleza ushirikiano Tz, Zambia

**Na Godfrey Sanga**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ametenga hekta 20 kwa Zambia katika Bandari Kavu ya Kwala iliyopo mkoani Pwani kwa ajili ya kuhudumia mizigo ya nchi hiyo inayoingizwa nchini na kusafirishwa nje ya nchi kupitia Bandari ya Dar es Salaam, huku akihimiza jumuiya ya wafanyabiashara nchini humo kutumia Bandari ya Dar es Salaam.

Amesema Bandari ya Dar es Salaam inafanyiwa maboresho makubwa kukidhi mahitaji makubwa ya kisasa na haraka zaidi ya usafirishaji mizigo.

Aliyasema hayo jana akiwa mgeni rasmi katika siku ya maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa Zambia, sherehe zilizofanyika jijini Lusaka na matangazo yake kurushwa moja kwa moja kupitia TBC1.

Alisema Zambia ni mteja mkubwa wa Bandari ya Dar es Salaam, ikichukua asilimia 34 ya mizigo yote inayopitia bandari hiyo kwenda nje ya Tanzania.

Rais Dk. Samia alitumia fursa hiyo kusema kwamba mipaka ya kijiografia baina ya Tanzania na Zambia, haipaswi kuwa kikwazo cha biashara na uwekezaji baina ya nchi jirani.

Akiipongeza Zambia kwa kumbukizi ya siku ya Uhuru wao, Rais Dk. Samia alisema anapenda kuona amani iliyopo kati ya nchi mbili hizo inaendelea kudumu.

Kauli mbiu ya siku hiyo ya Uhuru ni 'Kuchapusha Maendeleo ya Kitaifa kupitia Ugawanaji wa kupitiarasilimali zilizopo.'

"Tunapongeza juhudi zenu katika ushirikiano wa kikanda... tunapenda kuona kanda yetu na Afrika kwa ujumla, inakuwa na amani," alisema.

> **Rais Dk. Samia alitumia fursa hiyo kusema kwamba mipaka ya kijiografia baina ya Tanzania na Zambia, haipaswi kuwa kikwazo**

Aidha, alisema upembuzi yakinifu unaendelea kuhusu ujenzi wa bomba la gesi kutoka Tanzania hadi Zambia ikiwa ni moja ya mradi mkakati ambao ukikamilika utapunguza gharama za usafirishaji wa mafuta kwenda nchini humo na wamepanga kuimarisha bomba la mafuta la Tazama na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (Tazara). Kwa upande wake, Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, alisema Tanzania itaendelea kuwa mshirika mzuri kwa kuwa msingi wa mahusiano kati ya nchi mbili hizo, umejengwa na Baba wa Taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Baba wa Taifa la Zambia, Mzee Kenneth Kaunda.

Mapema asubuhi jana, Rais Dk. Samia na mwenyeji wake Rais Hichilema, walifanya dua na kuweka mashada ya maua kwenye mnara wa mashujaa uliopo Mtaa wa Uhuru Lusaka na waliweka pia mashada ya maua katika kaburi la muasisi na Baba wa Taifa hilo, Hayati Kenneth Kaunda.



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza jambo na mwenyeji wake, Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, wakati viongozi mbalimbali wakiweka mashada ya maua kwenye eneo la Mnara wa Kumbukumbu ya Wapigania Uhuru (Mashujaa) wa nchi hiyo katika maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa nchi hiyo jijini Lusaka jana. Picha: (Ikulu).**

# Milioni 1.6 kufanya mtihani darasa la 4

**Na Hellen Mwango**

WALIMU wakuu na wamiliki wa shule binafsi wametakiwa kufuata miongozo inayotolewa na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), wakati wanafunzi zaidi ya milioni 1.6 wanapoanza mtihani wa upimaji wa kitaifa wa darasa la nne leo.

Katika mtihani huo unaotarajiwa kumalizika kesho, wasichana waliosajiliwa ni 864,211 sawa na asilimi 51.05 na wavulana ni 828,591, sawa na asilimia 48.95.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Dk. Said Mohamed alisema wanafunzi wengine 759,573 wanatarajiwa kuanza upimaji wa kitaifa wa kidato cha pili Oktoba 30 hadi Novemba 9, mwaka huu.

Katika mtihani huo wa kidato cha pili wasichana ni 405,766 na wavulana 353,807.

Alisema shule za msingi 19,284 na shule za sekondari 5,546, zote za Tanzania Bara zinatarajia kufanya mitihani hiyo ya darasa la nne na wa kidato cha pili mtawalia.

Akifafanua kuhusu darasa la nne, Dk. Mohamed alisema waliosajiliwa kufanya upimaji mwaka huu ni 1,682,802 na kwamba miongoni mwa hao, wanafunzi 1,605,379 sawa na asilimia 94.84 watafanya upimaji kwa lugha ya Kiswahili na wanafunzi 87,423, sawa na asilimia 5.16 watafanya upimaji kwa lugha ya Kiingereza wanayoitumia katika kujifunzia.

Aidha alisema wanafunzi wenye mahitaji maalumu ni 6,402 na kwamba 1,074 kati yao ni wenye uoni hafifu, 93 ni wasioona, 1,240 wenye ulemavu wa kusikia, 2,209 ni wenye mtindio wa ubongo na 1,786 ni wenye ulemavu wa viungo vya mwili.

Kwa upande wa kidato cha pili, Dk. Mohamed alisema wanafunzi wenye mahitaji maalumu ni 1,382, ambapo wanafunzi 683 wana uoni hafifu, 82 ni wasioona, 290 wana ulemavu wa kusikia, 390 ni wenye ulemavu wa viungo vya mwili na 18 wana ulemavu wa akili.

"Maandalizi yote kwa ajili ya upimaji wa darasa la nne na kidato cha pili, yamekamilika ikiwamo kusambazwa kwa karatasi za upimaji pamoja na nyaraka zote muhimu. Walimu wakuu na wamiliki wanafahamu miongozo hivyo waifuate na kuizingatia," alisisitiza.

"Kamati za mitihani za mikoa na halmashauri zimefanya maandalizi yote muhimu kwa kutoa semina kwa wasimamizi wa mitihani pamoja na kuhakikisha mazingira ya vituo vya upimaji yapo salama, tulivu na kuzuia mianya yote inayoweza kusababisha kutokea udanganyifu," alisema.

Akifafanua zaidi alisema Baraza linatoa wito kwa wasimamizi wote walioteuliwa kusimamia upimaji kufanya kazi yao ya usimamizi kwa umakini, uadilifu, weledi na kwa kuzingatia kanuni za mitihani na miongozo waliyopewa ili kila mwanafunzi husika apate haki yake.




**Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania, Dk. Said Mohamed.**

"Baraza linatarajiwa kuwa wanafunzi watafanya upimaji kwa kuzingatia kanuni za mitihani na kwamba halitarajii kuona mwanafunzi yeyote akijihusisha na na vitendo vya udanganyifu," alisema.

Hata hivyo, alionya kwamba atakayebainika kufanya udanganyifu matokeo yake yatafutwa.

Alisema ni vyema wamiliki wa shule watambue kuwa shule zao ni vituo maalumu vya mitihani na kwamba hawatakiwi kwa namna yoyote ile kuingilia majukumu ya wasimamizi wa mitihani katika kipindi chote cha ufanyaji wa upimaji huo.

"Baraza halitasita kukifutia kituo chochote cha mtihani endapo litajiridhisha pasipo shaka kwamba uwepo wake unahatarisha usalama wa upimaji wa kitaifa. Wakuu wa shule watatekeleza majukumu yao ya usimamizi kwa kuzingatia mwongozo wa usimamizi uliotolewa na Baraza kuepuka kuingilia usimamizi wa wanafunzi ndani ya vyumba vya mitahani," alisema Dk. Mohamed.

Baraza limetoa wito kwa jamii kutoa ushirikiano katika kuhakikisha upimaji wa darasa la nne na wa kidato cha pili, mwaka huu unafanyika kwa amani na utulivu.

# Wakunwa uteuzi wa Makonda

**Na Mwandishi Wetu**

WATU mbalimbali wameendelea kupongeza uteuzi wa Paul Makonda kuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi wakisema kama ni upele umepata mkunaji.

Katibu wa Maendeleo ya Veterani wa Umoja wa Vijana wa CCM makao makuu ya ofisi ndogo Dar es Salaam, Kapteni Mstaafu, Mohamed Ali Ligora, alisema katika mahojiano jana kwamba uteuzi wa Makonda umefanyika kwa umakini mkubwa.

Halmashauri Kuu ya CCM Taifa katika kikao chake maalumu kilichokaa chini ya Mwenyekiti wa CCM, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kilifanya mabadiliko madogo ya Sekreterieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, kwa kumteua Makonda kuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi, Oktoba 22, mwaka huu.

Akizungumza na Uelekeo kwa njia ya simu jijini Dar es Salaam jana, Ligora alisema Kapteni mstaafu Ligora anasema Rais Dk. Samia ni chapa ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyekuwa Rais wa kwanza wa Tanganyika na baadaye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba ni chapa pia ya Rais Sheikh Abeid Aman Karume aliyekuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Alisema hali hiyo inatokana na jinsi anavyoendesha nchi kwa namna ambavyo Baba wa Taifa alitaka nchi iendeshweje na kwa namna ile ile ambayo Sheikh Karume alitaka nchi iendeshweje.

“Ndiyo maana nchi hizi zilizokuwa mbili zikaunganishwa kuwa nchi moja inayoitwa Tanzania kama walivyotaka Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume kwamba mtu mmoja mmoja katika nchi wawezeshwe na serikali kufikia hatua ya kujitegemea.

“Mfano hai, Mwalimu Nyerere aliwafikisha Watanganyika kuwa na viwanda na mashirika mengi huku akiwasomesha vijana kukidhi matakwa ya viwandas na mashirika;

“Kwa upande wa Sheikh Karume alipoambiwa na Waingereza kwamba watamsaidia kujenga maeneo ya kukaa wananchi kule Michenzani pale watakapomletea sampuli ya udongo waliouchukua kwenda kuupima yajengwe majengo ya aina gani na ya ghorofa ngapi, Sheikh Karume akaita Baraza La Mapinduzi kesho yake na kwenda kupima Michenzani aina ya majengo wanayotaka kujenga.

“Wataalamu tayari wawe na kamba za kupimia na mimi mwenyewe nitaanzisha upimaji huo,” alisema Ligora akimkariri Karume.

Anasema katika hali hiyo, Makonda ni wa Mwalimu Nyerere ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa Ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika na Mkombozi wa Makada maalumu wa nchi hizo, na kwa hiyo, Komredi Makonda ni mwanamapinduzi wa Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume ambaye ni Mkombozi wa Zanzibar.

“Mtazamo wangu ni kwamba, Komredi Makonda anamkidhi Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume kwa kukataa wananchi kunyanyaswa na kwa hiyo mwenye tabia ya kunyanyasa ndani ya CCM, Serikali na ndani ya wananchi watamwona Makonda ni hatari kwao.

“Lakini kwa mtazamo wa Samia alionao hao waliobaki walio wanyanyasaji ndani ya CCM, ndani ya Serikali na ndani ya wananchi watabadilika na nchi itasonga mbele kwa mwendo wa uhakika wa uchumi wa kujitegemea kwa kila mwananchi,” alisema.

Akitoa mfano, alisema baadhi ya wahitimu wa vyuo mbalimbali wameruhusiwa kujiunga makundi makundi na Rais Samia amewatayarishia maeneo ya kudumu kama makazi yao, vijiji vyao na sehemu ya uchumi wa aina mbalimbali.

Alisema katika hali hii ya kuwaona vijana ni aina ya tabia aliyofanya Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume ya kukabidhi vijana katika harakati za ukombozi wa Uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na kwa sababu hiyo ndiyo unavyoiona Tanzania ya leo inang’aa na barabara ya safari ya kuelekea kwenye kujitegemea kwa kila mwananchi iko wazi.

Anawataka wananchi, wana CCM na Jumuiya za CCM na Serikali za CCM kuendelea kuelewa kwamba mwendo wa Rais Dk. Samia ni kudra ya Mwenyezi Mungu na Watanzania wanamjua Mungu.

Naye wakili wa kujitegemea ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, alisema Rais amepiga kwenye mshono kwa kumteua Makonda katika nafasi maana sasa nazi imepata mkunaji.

Alisema hana mashaka kabisa na utendaji wa Makonda kwa sababu ni kijana mchapakazi na CCM inahitaji viongozi wa aina yake.

“Nazi imepata mkunaji sasa. Namaanisha CCM itarajie makubwa zaidi, atakipeleka chama mbele zaidi, ataendelea pale walipoishia watangulizi wake,” alisema.

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Vikongoro, Chanika, Seif Mwera alisema anampongeza Rais Dk. Samia kwa kumteua Makonda kwa kuwa kila mmoja kwenye chama anaelewa utendaji wake.

Alisema uteuzi huo unakwenda sambamba na kupokea kijiti cha mtangulizi wake kukipeleka chama mbali zaidi.

“Katika chama wengi tunamfahamu Makonda hasa sisi wakazi wa Dar es Salaam, alituongoza kwenye mkoa wetu vyema na sasa tunatarajia makubwa ndani ya CCM, anakijua chama vizuri Mama Samia anastahili pongezi kwa hili," alisema Mwenyekiti Mwera.

Mwandishi mkongwe, Hamisi Kibari alisema anamfahamu Makonda kama kiongozi mwenye kufikiri sana juu ya watu anaowaongoza, kukerwa na kero zao na kuthubutu kuziondoa.

“Alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kuna mambo mengi alifikiri, akathubutu kutaka kutatua kero mbalimbali hata kama si zote alizofanikiwa kuzitatua. CCM imeleta kwenye eneo hili la uenezi kijana anayefikiri,” alisema mwandishi huyo.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Paul Makonda




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

**Ndiyo maana nchi hizi zilizokuwa mbili zikaunganishwa kuwa nchi moja inayoitwa Tanzania kama walivyotaka Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume kwamba mtu mmoja mmoja katika nchi wawezeshwe na serikali kufikia hatua ya kujitegemea.**

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi


## HII NI KERO

### Vijana kuvamia siti za wenye mahitaji



KUNA baadhi ya vijana wamekuwa na tabia ya kuwapiga vikumbo watu wenye mahitaji maalum wakiwemo wazee, wajawazito, wenye ulemavu, waliobeba watoto na wagonjwa wakati wa kupanda mabasi ya mwendokasi.

Mabasi hayo yameweka utaratibu mzuri wa kutenga angalau viti vitano mahususi kwa makundi hayo, lakini vijana bila soni, hutumia nguvu zao kuwapiga vikumbo na kukimbilia kukaa kwenye nafasi hizo kisha kubandika masikioni `ear phones' na kujifanya `bize' kuchat na simu. Hii ni kero, vijana badilikeni!




## MAONI YA MHARIRI

# Kila la heri darasa la nne

KUANZIA leo na kesho, wanafunzi zaidi ya milioni 1.6 wa darasa la nne, wanatarajia kuanza mitihani wa kitaifa unaolenga kuwapima uwezo wao kabla ya kwenda darasa la tano.

Taarifa iliyotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) jana ilisema kwamba wasichana watakaofanya mtihani huo ni 864,211, sawa na asilimia 51.05 na wavulana ni 828,591, sawa na asilimia 48.95.

Hadi jana, kwa mujibu wa Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Dk. Said Mohamed, maandalizi yote kwa ajili ya upimaji wa darasa la nne nchini kote, yalikuwa ya mekamilika.

Mtihani huo wa darasa la nne utafuatiwa na mtihani mwingine wa upimaji wa kidato cha pili utakaoanza Oktoba 30 hadi Novemba 9, mwaka huu ukihusisha wanafunzi 759,573, ambapo wasichana 405,766 na wavulana ni 353,807.

Katika maandalizi ya mitihani hiyo miwili, Dk. Mohamed alisema kamati za mitihani za mikoa na halmashauri, zimefanya maandalizi yote muhimu kwa kutoa semina kwa wasimamizi wa mitihani hiyo pamoja na kuhakikisha mazingira ya vituo vya upimaji yapo salama, tulivu na kuzuia mianya yote inayoweza kusababisha kutokea udanganyifu.

Tunaipongeza serikali kuendeleza mitihani hii kwa sababu inasaidia wanafunzi wafanye marejeo ya kile walichojifunza katika madarasa au vidato vya nyuma.

Hatua ya kuwapima vijana wetu wakiwa katikati ya masomo kitaifa ni muhimu katika kuboresha kile wanachojifunza kuliko watoto wanaposoma kuanzia darasa la kwanza hadi la saba au kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne bila kupimwa.

Upimaji huu huwasaidia wanafunzi, wazazi, walimu, shule, halmashauri na wadau wengine kujua hali ilivyo ili kujipanga vizuri zaidi kwa ajili ya mitihani ya kuhitimu masomo, iwe ni ya shule ya msingi au ya sekondari.

Tunaamini kwamba walimu wakuu na wamiliki wa shule binafsi watafuata miongozo iliyotolewa na kuhakikisha mitihani katika shule zao inafanyika kwa utulivu na bila udanganyifu.

Halikadhalika tunaamini wasimamizi wote walioteuliwa kusimamia upimaji huu watafanya kazi yao ya usimamizi kwa umakini, uadilifu, weledi na kwa kuzingatia kanuni za mitihani na miongozo waliyopewa ili kila mwanafunzi afanye mtihani bila bughudha.

Tunaungana na Baraza kutoa wito kwa jamii yote ya Watanzania kutoa ushirikiano unaotakiwa katika kuhakikisha upimaji wa darasa la nne na kidato cha pili mwaka huu unafanyika kwa amani na utulivu.

Tunawatakia kila heri wote wanaoanza mitihani hiyo ya upimaji leo kwa maana ya darasa la nne, na wale wa kidato cha pili.


## Wasiliana nasi

| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255787559090 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |




Na Godfrey Sanga
Sangagodfrey26@gmail.com

## JICHO LANGU

# DP World manufaa kwa wote

OKTOBA 22, mwaka huu, mamilioni ya Watanzania, macho yao yalishuhudia utiaji saini Mkataba wa Uendeshaji wa Gati namba nne mpaka saba za Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza ufanisi katika bandari hiyo zoezi lililofanyika makao makuu ya nchi, Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alisimamia utiaji saini huo ambapo pia ulihhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, vyama vya siasa na viongozi wa dini.

Rais wa Zanzibar ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, alihudhuria hafla hiyo.

Aidha, Rais mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete na Waziri Mkuu mstaafu Federick Sumaye na Mizengo Pinda, walikuwepo.

Akizungumza baada ya kushuhudia utiaji saini wa mikataba hiyo, Rais Dk. Samia alisema kuwa hatua hiyo inafikiwa baada ya kufanya uchambuzi wa kina ikiwemo maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Watanzania wa kada mbalimbali.

Aidha, Rais Dk. Samia alisema uwekezaji unaofanywa na kampuni ya DP World, utabadilisha utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam na kuiwezesha kuchangia zaidi katika Pato la Taifa.

Moja ya faida kubwa ya uwekezaji huo ilielezwa kuwa kuongezeka kwa makusanyo kodi, ushuru wa forodha na tozo mbalimbali ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) itakusanya Sh. za Tanzania trilioni 26.7 kufikia mwaka 2032 tofauti na sasa ambapo mamlaka hiyo inakusanya Sh. trilioni 7.8 kwa mwaka.

Licha ya hatua hii nzuri iliyofikiwa na serikali, bado kuna baadhi ya Watanzania wanaotilia shaka mikataba hii wakiona pengine kuna vipengele vilivyofichika ndani yake.

Hata hivyo, serikali haikusita kubainisha mengi ya masuala yaliyokuwa na utata mwanzoni ikiwemo kubwa zaidi kuwekwa muda wa ukomo wa mkataba miongoni mwa mengine.

Utamkumbuka, Mchumi na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala tawi la Dar es Salaam, Dk. Bravious Kahyoza, aliwahi kukaririwa na vyombo vya habari akieleza kuwa ipo hatari ya kubinafsisha viungo vikuu vya uchumi kama Bandari kwa wawekezaji binafsi.

Moja ya manufaa ya uwekezaji huo ni pamoja na kuongeza ufanisi kwa huduma zitakazotolewa kwa meli na shehena kupita katika Bandari ya Dar es Salaam.

Pia utaboresha huduma katika Bandari ya Dar es Salaam kwakupunguza muda wa kuchakata nyaraka kwa kuwa kampuni ya DP World itatumia mifumo ya kisasa ya Tehama itakayofungamanishwa na wadau wote wa bandari.

Watanzania wanaiunga mkono serikali katika uwekezaji huu kwani wanaona mazuri na makubwa yanayokuja kwa siku za usoni. Ewe mdau, afisa, mama, baba na mzalendo yeyote wa nchi hii, muhimu kutambua kuwa utendaji shirikishi wa haki na kujituma ndiyo ufanisi bora utakaoleta matokeo mazuri kwa wote.

> **Watanzania wanaiunga mkono serikali katika uwekezaji huu kwani wanaona mazuri na makubwa yanayokuja kwa siku za usoni. Ewe mdau, afisa, mama, baba na mzalendo yeyote wa nchi hii, muhimu kutambua kuwa utendaji shirikishi wa haki na kujituma ndiyo ufanisi bora utakaoleta matokeo mazuri kwa wote.**

Kazi Iendelee.

## MKATABA TPA NA DP WORLD:

# Samia athibitisha usikivu na utekelezaji




**Na John Ngunge**

LICHA ya Bandari ya Dar es Salaam kuwa lango la biashara, pia ni maliasili, ni jaha, ni hidaya adhimu ambayo Taifa imejaaliwa na Mwenyezi Mungu, anasema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Anaongeza, kuumbwa kwa bandari hii na kuwekwa Tanzania kunaipatia taifa wajibu wa kuhudumia nchi jirani wanaoitegemea. Hii ni kwa mujibu wa makubaliano ya Almaty ya Umoja wa Mataifa, (Almaty Programme of Action) kwa nchi zenye mlango bahari yaani bandari.

Anakumbusha kuwa nchi hizo zina wajibu wa kuhudumia na kuhakikisha ustawi wa nchi zisizo na milango bahari.

Katika kutekeleza wajibu huo, Rais Dk. Samia anasema Serikali imewekeza sana kwenye kuiunganisha nchi yetu na nchi zinazotuzunguka kupitia barabara, vituo vya utoaji huduma mipakani, reli, usafiri wa majini, na imeendelea kuboresha bandari zetu za kwenye maziwa kama Mwanza, Kigoma na Karema na hata usafiri wa angani.

Anabainisha kuwa ununuzi wa ndege ya kwanza ya mizigo iliyowasili nchini hivi karibuni utasaidia kupeleka mizigo inayotoka bandarini kwenda nchi jirani hasa ile inayohitaji usafiri wa haraka.

Hivyo, anasema ni lazima kukuza uwezo na ufanisi wa bandari yetu ili iweze kusafirisha mizigo mingi zaidi ili kukamilisha mnyororo wa biashara na nchi majirani zetu.

Kwa kuzingatia ukweli huo, anasema busara iliwaelekeza wapate mwekezaji ambaye watashirikiana naye si tu katika kujibu changamoto za upatikanaji wa mizigo au mzigo wa kutosha wa kuingia na kutoka nchini, vile vile kuongeza ufanisi utakaofanya gharama kuwa shindani na bandari nyingine katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Anasema walizingatia pia ukweli kuwa Bandari ya Dar es Salaam siyo mlango bahari pekee Mashariki na Kusini mwa Afrika kwani kuna milango bahari mitatu ya Mombasa, Beira na Durban na kwa upande wa Magharibi kuna milango bahari ya Walvis Bay nchini Namibia na Lobito nchini Angola, hii ikiwa na maana kwamba wale wanaotaka mizigo yao ifike wana uwezo wa kuchagua bandari yoyote wakaitumia.

Lakini anasema; "Kinachotupa sisi turufu dhidi ya washindani wetu ni bahati ya mlango wetu wa bahari kuwa na masafa mafupi kuingia nchi jirani na kwamba tunafikika na nchi nyingi kwa kutumia mpaka mmoja tu tofauti na milango bahari mingine.

"Hata hivyo, ukaribu peke yake siyo hoja ya kutosha kwa sababu kama ukaribu tumekuwa nao siku zote hivyo lazima tufanye kazi ya kuongeza ufanisi katika bandari yetu kwa sababu wafanyabiashara hutazama ufanisi na gharama," anasema.

**Pia tuliangalia maoni katika mitandao ya kijamii. Tumewasikiliza viongozi wetu wa dini na baadhi ya viongozi wetu wastaafu. Mikataba ya Uwekezaji wa Bandari iliyosainiwa imezingatia maoni yaliyotolewa kupitia makundi mbalimbali ya kijamii, pamoja na sheria na taratibu za nchi.**

Busara ya Serikali anayoingoza Rais Dk. Samia ndiyo iliyofikia maamuzi ya kusaini mikataba mitatu kati ya kampuni ya DP World ya Dubai, kuhusu uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam.

Hatua hii imeendelea kuthibitisha kuwa serikali anayoiongoza ni sikivu na inatekeleza ahadi zake. Pia ni serikali inayojali maslahi ya taifa na wananchi wake.

Mikataba hiyo iliyosainiwa Oktoba 22, mwaka huu, katika hafla iliyofanyika Ikulu ya Chamwino, jijini Dodoma, ilihusu uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam pekee inahusisha upangishaji na uendeshaji wa Gati namba 4 hadi 7.

Mikataba hiyo ni Mkataba wa Nchi Mwenyeji; Mkataba wa Upangishaji Ardhi na Mkataba wa Uendeshaji wa Bandari.

Mikataba hiyo kwa mujibu wa Rais Dk. Samia, imetokana na makubaliano ya awali kati ya Serikali na Mamlaka ya Dubai ambao wameridhia mahitaji na matakwa ya nchi kama yalivyosainishwa kwa kuzingatia maslahi ya taifa.

Kauli ya Dk. Samia ambayo aliitoa baada ya kushuhudia utiaji saini wa mikataba hiyo, imeendelea kudhihirisha kwamba ni Rais Samia ni msikivu anayejali wananchi wake.

Tangu Juni, mwaka huu, baada ya Bunge kuridhia mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa Bandari Tanzania (IGA), Serikali ilitoa fursa kwa wananchi kutoa maoni yao.

Maoni hayo yalitolewa na mtu mmoja mmoja, makundi ya watu, taasisi za dini, wabobezi au manguli wa fani mbalimbali, na Serikali ilisema itasikiliza na kuzingatia maoni hayo, na kwa kweli imetekeleza.

Baada ya uchambuzi wa maoni ya wadau kama yalivyowasilishwa serikalini kwa njia mbalimbali, zikiwemo rasmi au kwa kutumia mitandao ya kijamii, hatimaye wakati wa kusaini mikataba hiyo, Rais Dk. Samia alidhihirisha ukweli kwamba ni msikivu.

Kuthibitisha usikivu wake, Rais Dk. Samia kwa kauli yake aliyoitoa baada ya kushuhudia utiaji saini wa mikataba hiyo, alisema:

"Serikali kwa upande wake ilisikiliza michango na maoni mbalimbali yaliyotolewa na Chama cha Wanasheria wa Tanganyika, vyama vya siasa, asasi za kiraia, wanaharakati huru na vyombo vya habari.

*Inaendelea Uk. 8*

# Samia athibitisha usikivu na utekelezaji

*Inatoka Uk. 7*



''Pia tuliangalia maoni katika mitandao ya kijamii. Tumewasikiliza viongozi wetu wa dini na baadhi ya viongozi wetu wastaafu. Mikataba ya Uwekezaji wa Bandari iliyosainiwa imezingatia maoni yaliyotolewa kupitia makundi mbalimbali ya kijamii, pamoja na sheria na taratibu za nchi."

Kwa kifupi, hatua ya kufikia kusaini kwa mikataba hiyo unadhihirisha kuwa mchakato wake ulikuwa shirikishi tangu mwanzo wa majadiliano mpaka sasa katika uingiaji wa mkataba wa utekelezaji.

Amesema mchakato wa majadiliano ya uingiaji mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na DP World katika uendelezaji na uendeshaji wa bandari ya Dar es Salaam umekuwa shirikishi tangu mwanzo wa majadiliano mpaka hatua ya utiaji saini.

Rais Dk. Samia akiwa pamoja na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliongoza makumi kwa mamia ya Watanzania walioalikwa Ikulu Chamwino jijini Dodoma kushuhudia utiaji saini wa mikataba hiyo.

Mihimili yote mitatu ya Utawala, Bunge na Mahakama ilikuwepo kushuhudia tukio hilo la kihistoria likiandikwa.

Walioalikwa waliwakilisha taasisi zao kama vile CCM, viongozi wa vyama vya siasa, taasisi binafsi, viongozi wastaafu na viongozi wa dini.

Mamilioni ya Watanzania wengine walishuhudia hafla hiyo kupitia matangazo ya televisheni (na njia zingine za mitandao ya kijamii) yaliyorushwa moja kwa moja na kusikika sehemu mbalimbali nchini na duniani kote.

Mikataba hiyo mitatu imesainiwa kwa kuzingatia Kifungu cha 2 cha Sheria ya Ubia Namba 6 ya mwaka 2023 na Kifungu cha 2 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 5 ya mwaka 2023, inakwenda kuongeza mapato ya serikali, hivyo kukuza uchumi wa taifa.

"Kwa uhakika hakuna sauti au kundi ambalo halikusikilizwa au kupuuzwa. Serikali tuliunda jopo la wataalamu, pia wanasiasa na wanasheria waangalie hoja zote na watuambie ipi iingie kwenye mkataba na ipi haina mashiko," alisema.

Anasema mikataba hii imezingatia maoni yote yaliyotolewa, na pia maslahi mapana ya nchi yetu.

Anasema kilichofanyika katika uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam ni kuhakikisha bandari hiyo inaendeshwa katika viwango vinavyokubalika duniani, kukuza ufanisi na biashara na hatimaye kukuza mapato ya nchi.

Akibainisha mambo 10 muhimu yanayohusu mkataba wa uwekezaji na uendelezaji kati ya Serikali na kampuni ya DP World ya Dubai, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa, anasema, mikataba hiyo imezingatia vitu vingi ndani yake kwa maslahi mapana ya nchi.

Ametaja mambo hayo 10 kuwa ni mikataba kuhusisha baadhi ya magati ya Bandari ya Dar es Salaam na sio maeneo yote ya Bandari ya Dar es Salaam na mikataba hii haihusishi bandari nyingine za mwambao na maziwa.

Anasema mkataba huu una ukomo wa miaka 30 na utakuwa ukirejewa kila baada ya miaka mitano ikiwa ni pamoja na kurejea mpango wa uwekezaji; kuwa na kampuni ya uendeshaji ambayo TPA itamiliki hisa na kuweka viwango vya utendaji ambazo mwekezaji anapaswa kuvifikia.

Mengine ni kwa watumishi wa sasa wa TPA kupewa nafasi ya kuchagua kubaki TPA au kuhamia kwa mwekezaji, na kwamba jukumu la ulinzi na usalama katika eneo lote la bandari na yaliyokodishwa kwa DP World yataendelea kubaki Serikalini.

Mbossa anasema mwekezaji atatakiwa kulipa kodi na tozo zote za Serikali kwa kuzingatia Sheria za Tanzania; kutumika kwa Sheria za Tanzania katika utekelezaji wa mikataba hii, kuwa na fursa za Watanzania kushiriki katika uwekezaji huu kupitia vifungu vya sheria vinavyolinda maudhui ya ndani ya nchi na kwamba imezingatia kuwepo kwa haki ya serikali kujiondoa katika mikataba hiyo.

Moja ya faida kubwa ya uwekezaji huo imeelezewa kuwa ni kuongezeka kwa makusanyo kodi, ushuru wa forodha na tozo mbalimbali ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) itaweza kukusanya Sh. Trilioni 26.7 kufikia mwaka 2032 tofauti na sasa ambapo mamlaka hiyo inakusanya Sh. Trilioni 7.8 kwa mwaka.

Kwa upande wake Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya DP World, Sultan Ahmed Bin Sulayem alisema katika miaka mitano ya mwanzo DP World itawekeza Dola za Marekani milioni 250 huku kazi ya kwanza ikiwa ni kuboresha miundombinu ya kushughulikia mizigo kwa haraka ili kuondoa kero ya ucheleweshaji wa mizigo unaoikabili Bandari ya Dar es Salaam hivi sasa.






*Leo ndiyo, kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu kuu

Jumatano Okt. 25- 31, 2023




*Jarida hili haliuzwi*

# Rais Samia aziunganisha Mbeya, Singida kwa lami



UK. 12 & 13



UK. 14

## Maisha, maajabu na uwezo wa mnyama nungunungu

## Uzushi umepata majibu ya kisayansi sakata la Bandari

UK. 11



Siasa

# Biteko ametoa darasa zuri kwa wanasiasa wetu

**Na Reubeni Lumbagala, Dodoma**

MWANAFALSAFA na mwanasiasa ambaye dunia itaendelea kumkumbuka kwa muda mrefu, Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema kuwa ili nchi iendelea inahitaji vitu vinne; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Uwepo wa vitu hivi vinne na mfumo madhubuti wa kuratibu, ni dhahiri maendeleo ya kweli yanayogusa maisha ya watu yataweza kufikiwa.

Lengo la makala haya ni kuangazia jambo moja kati ya hayo manne yaliyoainishwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere - Siasa safi.

Siasa inaweza kutafsiriwa kama matendo yanayohusiana na kuongoza pamoja na kufanya maamuzi kama vile mgawanyo wa raslimali katika ngazi mbalimbali za jamii, kama vile mji, taifa, au hata dunia nzima (siasa ya kimataifa).

Tofauti na wengi wanavyoitafsiri kwamba siasa ni uongo au porojo lakini ukweli ni kwamba siasa ni maisha. Siasa inagusa kila eneo la maisha ya kawaida ya kila siku ya mwanadamu. Wanasiasa ndio wanaotoa maamuzi ya mambo mengi yanayoendesha maisha yetu.

Hakuna namna ambayo ustawi na maendeleo ya watu unaweza kujadiliwa na kufikiwa bila uwepo wa siasa tena siasa safi yenye tija kwa wananchi. Kama kuna siasa safi basi jua pia kuna siasa chafu zisizo na manufaa kwa wananchi.

Kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya wanasiasa nchini kushindwa kufanya siasa safi zenye kugusa maisha ya wananchi, badala yake kujikita katika kutoa lugha za kebehi, dharau na zisizo na staha au kutaka kutumikiwa badala ya kuwatumikia wananchi. Siasa safi ni siasa zenye kujenga hoja, zenye kujikita kujibu mahitaji ya wananchi.

Oktoba 11, 2023 akiwa mgeni rasmi katika mkutano wa wanachama na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko alitoa darasa zuri la siasa safi kwa wanasiasa.

Mkutano huo ulioandaliwa na Mbunge wa jimbo hilo, Ridhiwani Kikwete, uliopokea taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM jimboni Chalinze.

Katika hotuba yake, Dk. Biteko alisisitiza kwamba ili kuwa na maendeleo ni vyema kufanya siasa zinazolenga kubadili maisha ya watu badala ya siasa za maneno.

"Shikamaneni, thaminianeni na kuvumiliana. Angalieni yanayowakeka pamoja badala ya yale yanayowatenganisha. Tusiingie kwenye matusi na kejeli. Kazi yetu iwe ya kuyasemea yale yaliyofanywa na serikali. Wananchi wanachohitaji ni huduma tuwapelekee maendeleo huko waliko raslimali fedha zilizopo zitumike kwa kiwango kinachotakiwa," alisisitiza Dk. Biteko.

Haya ni maneno mazito na darasa maridhawa kwa wanasiasa. Hii ni shule kamili kutoka kwa Dk. Doto Biteko.

Naibu Waziri Mkuu hiyo, anafahamu wanachotaka wananchi ni utatuzi wa kero zao na kutendewa au kupewa miradi inayogusa maisha yao.

Utatuzi wa kero za wananchi, unategemea utendaji kazi madhubuti na uadilifu wa viongozi waliopewa dhamana ya kuwatumikia wananchi.

Kimsingi, ukishakuwa kiongozi wa kuchaguliwa, kuteuliwa au kuajiriwa kwenye ofisi ya umma, wewe una dhima ya kuwajibika moja kwa moja katika kuwatumikia wananchi kwenye ofisi au eneo lako la kazi.

Baadhi ya dini kama Uislamu zinafundisha kwamba kila kiongozi hata kwa ngazi ya familia ni mchunga na mbele ya haki ataulizwa na Mwenyezi Mungu namna alivyochunga kondoo anaowaongoza.

Kwa mujibu wa mafundisho hayo, miongoni mwa watu saba watakaopata kivuli cha Mwenyezi Mungu siku ya kiama ni pamoja na kiongozi mwadilifu, anayejitoa na kuwatumikia wananchi kwa haki na kwa dhati.

Kwa hiyo, viongozi wanawajibika moja kwa moja katika kufanya siasa zitakazobadili maisha ya watu ili kuchochea maendeleo katika jamii na nchi kwa ujumla. Na wajue Wana maswali ya kujibu mbinguni.

Tatizo la baadhi ya viongozi ni kutumia madaraka au ofisi za umma kwa maslahi binafsi.

Dk. Biteko anataka kasi ya uboreshaji wa huduma za kijamii kwa wananchi iwe kubwa kwani hiyo ndiyo siasa safi yenye kubadili maisha ya watu.

Wananchi wanataka huduma bora za kijamii kama vile elimu, afya, maji, umeme, barabara, mawasiliano na nyinginezo.

Na kimsingi, nafsi au moyo wa mtu umeumbwa kumpenda anayempenda na kuonesha heshima kwake. Kwa hiyo kila kiongozi anayependa kukumbukwa, kuacha alama na hata kuombewa mazuri anapaswa kuwatumikia kwa uadilifu na haki wananchi.

Wananchi wanahitaji kuboreshewa shughuli zao, mathalani, uhakika wa kupata pembejeo kwa ajili ya kilimo, mifugo an uvuvi na kutembelewa na maofisa ugani ili walime kilimo chenye tija.

Vilevile, wananchi wanayo kiu ya kuboreshewa miundombinu ya barabara na ujenzi wa masoko ili waweze kufanya biashara zao katika mazingira mazuri ili hatimaye waweze kupata kipato kwa ajili ya familia zao na kuchangia maendeleo ya nchi yao.

Kufanikiwa kwa haya yote kunategemea utendaji kazi wa viongozi na watumishi wa umma wenye dhamira ya dhati ya kubadili maisha ya watu wanaowaongoza na kuwatumikia.

Aidha, Dk. Biteko anatoa rai juu ya matumizi mazuri ya fedha za umma zinazotengwa na serikali katika kughramia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Hii ni kutokana na ukweli kuwa kubadili maisha ya watu kunakwenda sambamba na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi ambapo bila matumizi mazuri ya fedha hizo, miradi hiyo itakwama na hivyo maisha ya wananchi yataendelea kuwa duni.

Hivyo basi, mkazo wa Dk. Biteko wa kutaka fedha za miradi zitumike kwa kiwango kinachotakiwa ni namna bora ya kufanikisha mkakati wa serikali wa kubadili maisha ya wananchi wake kutoka maisha ya chini hadi maisha bora.

Ni vyema ieleweke kwa wanasiasa kwamba kutaka kuungwa mkono na wananchi bila kuwa na mikakati thabiti inayopimika ya kubadili maisha ya wananchi ni kupoteza muda tu.

Wananchi wa sasa wanajua aina ya kiongozi wanayemtaka ili washirikiane nae katika juhudi za kujiletea maendeleo. Kiongozi huyo ni yule anayefanya siasa zenye mrengo wa kuboresha maisha yao, mwadilifu na asiye mbinafsi.

Kuhusu ubinafsi, wataalamu wa saikolojia wanasema kimsingi kila mtu anazaliwa akiwa na 'vinasaba' vya kujipendelea, yaani 'mimi kwanza' lakini uungwana na ustaarabu unapaswa kumsukuma mtu kukandamiza nafsi yake ili kuwajali watu wengine kwanza.

Ushirikiano na mshikamano vilevile ni moja ya msingi muhimu wa kufanya siasa safi. Viongozi ni lazima washirikiane kikamilifu na wananchi wao ili kuunganisha nguvu pamoja na hatimaye kufikia maendeleo ya kweli.

Pengine, ni muda mwafaka sasa kwa wanasiasa na wote waliokabidhiwa ofisi za umma ambao hawajashtuka kubadili mienendo na namna wanavyoendesha siasa.

Wajue kwamba wakati na mazingira ya siasa nchini yamebadilika. Kiongozi ni mtu wa kuwatumikia wananchi au kwa lugha nyingine ni mtumwa wao. Yule anayewania madaraka ya kisiasa akidhani yeye atakuwa bwanamkubwa na wananchi ni watu wa kumtumikia au kusukumasukuma 'amebugi stepu' kama wanavyosema vijana wa kisasa.

Ni lazima wanasiasa wajikite katika siasa safi kama alivyotoa darasa Dk. Biteko kwani bila kufanya hivyo, wataangukia pua.

Nimalizie kwa kumrejea tena Mwalimu Nyerere aliyepata kusema kwamba mtu mwaminifu na mwadilifu kabisa kabisa hakimbilii uongozi kwa sababu kila tatizo kwenye eneo lake la uongozi ni mzigo wake. Viongozi jueni kero na matatizo ya Watanzania ni mzigo wenu.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Mlali Sekondari ya mkoani Dodoma. Mawasiliano yake ni 0620 800 462.***

**Shikamaneni, thaminianeni na kuvumiliana. Angalieni yanayowakeka pamoja badala ya yale yanayowatenganisha.**



Kolamu

Hamisi Kibari
TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA
Simu: 0758143457

# Uzushi umepata majibu ya kisayansi sakata la Bandari

**Na Hamisi Kibari**

HATUA iliyofikiwa Jumapili kwa serikali kutia saini mikataba ya uendelezaji na uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam, imedhihirisha kwamba tuna Amiri Jeshi shupavu, muungwana, mtulivu na mvumilivu, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Lakini sakata hili la kuleta tena sekta binafsi katika kuendesha Bandari ya Dar es Salaam limesaidia pia kuonesha kwamba kuna tatizo la wanasiasa kuwabishia wataalamu wenye data huku wao wakiongozwa na mihemuko ya kisiasa.

**BANDARI YA DAR ES SALAAM**

Kimsingi, Bandari ya Dar es Salaam ni neema kubwa ambayo Mwenyezi Mungu ametupa Watanzania. Niliwahi kufanya mahojiano na Mkurugenzi Mkuu wa zamani wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Deusdedit Kakoko, akaniambia Bandari ya Dar es Salaam inapokea na kusafirisha takribani asilimia 90 ya mizigo yote inayoingia au kutoka.

Bandari nyingine ukiacha za kwenye maziwa ni ya Tanga na Mtwara ingawa kuna bandari ndogo za Lindi, Kilwa, Bagamoyo na Pangani.

Kwamba Tanzania ndiyo nchi inayopakana na nchi nyingi zisizo na bandari (land-locked countries) pengine kuliko nchi yoyote Afrika na hivyo ufanisi wa bandari hii una manufaa makubwa kwa Tanzania na nchi zinazoitegemea.

Nchi zisizo na bandari zinazotuzunguka ni pamoja na Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Lakini ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam unaweza kusababisha itoe huduma katika nchi zenye bandari ndogo kama Msumbiji na Madagascar na pia katika nchi za Sudan Kusini na Zimbabwe.

Kakoko akazidi kusema kwamba takribani asilimia 50 ya makusanyo ya Mamlaka ya Mapato nchini, yanatokana na Bandari ya Dar es Salaam na kwamba tukijipanga vizuri, Tanzania inaweza kuwa miongoni mwa nchi zinazotegemea bandari kwa zaidi ya asilimia 90.

**KWA NINI TUKO NYUMA?**

Kama sisi tuna nafsi ya kuhudumia nchi nyingi kuliko hata majirani zetu wa Kaskazini, kwa nini wao wanatuzidi ufanisi?

Zipo sababu kadhaa, miongoni mwa hizo ni pamoja na uwekezaji mdogo uliofanyika ambao hautoi ufanisi mkubwa.

Lakini kuna sababu za udhaifu na weledi wa menejimenti, wizi na hata kuhujumiwa au kuzidiwa ujanja na washindani wetu.

Niliwahi kuibiwa siri na mtu mkubwa bandarini hapo kwamba wanasiasa na sisi wanahabari, tumeshiriki sana `kuiua' Bandari ya Dar es Salaam bila kujua.

Kwamba kutokana na madudu yaliyokuwa yakifanyika, bandari iligeuka pia kuwa eneo la wanasiasa kujichukulia `ujiko' kwa kufichua uozo.

Hilo likitokea, sisi wanahabari ndiyo inakuwa habari yetu kubwa. Kumbe washindani wetu wakawa wanatunza zile habari (cuttings), kisha wanazitumia kama ushahidi kuwavuta wateja kwamba Bandari ya Dar es Salaam, ni madudu matupu!

Roho iliniuma sana niliposikia kwamba tulipokuwa na idadi kubwa ya wakimbizi, shirika moja la Kimataifa, lilikuwa linapitishia nchi jirani misaada kwenda kwa wakimbizi walio nchini mwetu badala ya Dar es Salaam baada ya kuaminishwa kwamba bandari yetu ni ya hovyo.

Nitumie wasaa huu kuweka angalizo kwamba matatizo kwenye maeneo nyeti kama bandari au utalii, ni ya kutatua kimya kimya na si kuita vyombo vya habari!

Takwimu zilizopo zinaonesha kwamba wakati bandari yetu hii kubwa ina uwezo wa kuhudumia tani milioni 25 pekee kwa mwaka, bandari za kisasa zinakwenda hadi tani milioni 100. DP World wana uwezo wa kutusogeza huko.

Bandari kwa sasa inaweza kuhudumia meli za kizazi cha pili zinazobebea hadi makontena 2,500, lakini haiwezi kuhudumia meli za kisasa za Post Panamax zenye uwezo wa kubeba makontena 8,000.

Bandari yetu inategemea wadau wengine kama ICDs na CFS kutunza na kuhudumia shehena, lakini bandari za kisasa huduma za UCD na CFS, zinapatikana kwenye bandari na hivyo kuokoa muda.

Wakati bandari yetu inahudumia makontena 12 kwa saa, bandari za kisasa huhudumia makontena 40 kwa saa. Wakati muda wa makontena kukaa bandarini ni siku saba, kwingineko ni chini ya hapo.

Lakini pia kwa sasa gharama za kupitishia mzigo Bandari ya Dar es Salaam, ni kubwa kwa sababu mbalimbali zikiwemo za meli kusubiri nangani muda mrefu na kuna mianya mingi ya kuombana rushwa.

Hata kwa viwango vya kimataifa vya utendaji (Port Performance Index - CPPI), bandari yetu imekuwa iko mkiani. Kwa mfano, katika viwango ambavyo hutolewa na Benki ya Dunia, kwa mwaka 2022, ilikuwa ya 361 kati ya bandari 386, yaani ilizidi bandari 25 tu. Mwaka huu 2023 ni ya 312 kati ya bandari 348 zilizokaguliwa. DP World wana uwezo wa kutusogeza nafasi za juu.



**KWA NINI TUSIWEKEZE WENYEWE?**

Swali kwa nini tusiwekeze wenyewe linafanana sana na wale ambao huwa wanauliza kwa nini tunakopa kujenga barabara, reli au mitambo ya kuzalisha umeme.

Jibu ni kwamba uwiano wa mapato na makusanyo huwa hauruhusu kutumia mapato kujenga kitu kama barabara ya kuunganisha mkoa na mkoa sambamba na kuendelea kuhudumia mahitaji mengine ya nchi.

Kwa kutegemea mapato ya ndani, kwa mfano, tunaweza kutumia miaka 20 kujenga barabara ili kuhakikisha shughuli nyingine za nchi ikiwemo kulipa mishahara ya watumishi wa umma hazikwamki.

Katika mazingira kama hayo, ni bora tukope, tujenge barabara katika kipindi kifupi kisha tuwe tunalipa deni taratibu huku tukiendela kutumia barabara.

Kama huwezi kukopa au kujenga barabara kwa miaka 20 kwa kutegemea fedha za ndani, uamuzi mwingine ni kuacha kabisa kujenga barabara na kuwa kama wenzetu wa DRC ambako unaweza kukuta hakuna kabisa barabara ya kuunganisha mkoa kama Morogoro na Dodoma, hivyo njia kuwa ya ndege pekee au kutumia punda!

**USHUPAVU WA SAMIA**

Ni dhahiri Bandari ya Dar es Salaam kwa kulinganisha na nyingine hata za majirani zetu, iko nyuma kiufanisi.

Badala ya kuendelea kukopa ili tuwekeze kwenye huu `mgodi' wetu muhimu sana katika kuiingizia nchi maokoto na badala ya kuendelea kuumiza kichwa kuhusu endeshaji wa kisiasa na kuifanya Bandari ya Dar es Salaam kuwa shindani, Rais Samia amekuja na njia rahisi ya kukaribisha mwekezaji mwenye sifa stahiki.

Wataalamu wake wamefanya tafiti, wamekwenda maeneo mbalimbali ya dunia ambako mwekezajihuyu DP World anaendesha bandari na kujiridhisha kwamba kama ni upele, huyu ndiye anaweza kuukuna.

DP World ni dude kubwa lenye uwezo na uzoefu wa kuendesha bandari, si katika Afrika na Mashariki ya Kati pekee, bali hata Ulaya.

Rais Samia angeweza kufanya uwekezaji huu kimyakimya kama ambavyo watangulizi wake wamekuwa wakifanya ikiwemo Kampuni ya Kimataifa ya Kuhudumia Shehena za Kontena Bandarini (TICS), lakini yeye ameleta uwazi na kuruhusu mijadala ya wazi.

Hatua ya Jumapili bila shaka imehitimisha hili na kuonesha mbivu na mbichi. Imemaliza uzushi katika hili.

**Kazi endelee.**

Siasa



Serikali pia imefanya ujenzi wa daraja kubwa la Itembe lenye urefu wa mita 150 pamoja na mradi kabambe wa kuunganisha Mikoa ya kanda ya ziwa, kanda ya kati na Kaskazini kuanzia Karatu mpaka Mbulu...

# Rais Samia aziunganisha Mbeya, Singida kwa lami

## ■ Atandika mkeka wa Kilomita 413, atumia bilioni 67

**MOJA ya njia kubwa ya kukuza uchumi ni suala la miundo mbinu. Sehemu yoyote ambayo haifikiki kwa urahisi inakuwa ngumu maendeleo kufika katika eneo hilo. Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imegundua hilo na kuamua kuweka katika ujenzi wa Barabara na madaraja ili kuhakikisha uchumi wa wananchi unapanda. Katika Makala haya, Mwandishi Wetu Petter Mwendapole anaangalia juu ya uwekaji na uzinduzi wa barabara katika mkoa ya Singida ambayo inaunganisha mpaka Mbeya, huku Dodoma, Tabora zikifaidika.**

MIKOA ya Mbeya na Singida kwa sasa inaweza kufikika kwa urahisi zaidi ambapo ndani ya masaa matatu na nusu unaweza kufika kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Zaidi ya Kilomita 400 zimejengwa kwa kiwango cha lami na hivyo kufanya biashara katika maeneo hayo kufanyika kwa urahisi zaidi. Hii inamaanisha kuwa hata mazao au wafanyabiashara wanaotaka huduma katika mikoa hiyo miwili wataweza kufanya kazi zao kwa urahisi na ufanisi.

Oktoba 15 mwaka huu, Dk. Samia Suluhu Hassan aliweka jiwe la msingi katika mradi wa barabara Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa ambapo barabara hiyo una Kilometa 413.

Lakini pia Rais Samia aliweka pia jiwe la ujenzi wa sehemu ya Mkiwa – Itigi –Noranga yenye urefu wa kilometa 56.57.

Akizungumza na Wananchi wa Itigi Mkoani Singida katika Uwanja wa Police Square, Rais Samia amesema barabara hiyo ya kiwango cha lami inajengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 67.2 na dola za Kimarekani milioni 1.01.

"Ujenzi wa barabara hii utatuunganisha na Ushoroba wa Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM Highway) na Ushoroba wa Barabara Kuu ya Kati (Central Corridor) eneo la Mkiwa katika barabara ya Dodoma – Singida kwa hiyo barabara hiyo ina umuhimu mkubwa sana kwa Mkoa wa Singida,

Mbeya, Tabora pamoja na Kanda mbalimbali zinazounganisha Nchi yetu na Ukanda wa SADC.

"kukamilika kwa barabara hiyo kutachochea shughuli za uzalishaji na biashara kwa kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa za Kilimo, Madini na Misitu," amesema.

Dk. Samia amesema kutokana na umuhimu wa barabara hiyo serikali inaangalia uwezekano wa kuijenga bila kusimama kwa kuipeleka mpaka Makongolosi ambapo itaunganisha Mkoa wa Mbeya ili biashara iweze kushamiri baina ya Mbeya na Singida.

Katika kuhakikisha hilo linafanyika kwa uhakika, amemuagiza Waziri wa fedha Dkt Mwigulu Nchemba na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa kusimamia suala hilo.

Rais Dkt. Samia amesisitiza kuwa Serikali imejidhatiti kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja nchini kote.

Rais ametaja miradi ambayo serikali imeikamilisha hivi karibuni katika ukanda wa kati ikiwemo daraja la Sibiti lenye mita 82, Manyoni – Itigi – Chaya km 85, Tabora -Nyahua -Chaya km 166.5, Tabora- Koga – Mpanda km 360, Nzega – Tabora km 116, Tabora – Ndono – Urambo km 87, Dodoma – Mayamaya - Mela km 47, Mwigumbi – Maswa km 50.5, Maswa- Bariadi km 50 na Bariadi – Lamadi km 71.

"Miradi mingine inayoendelea kujengwa ipo katika hatua mbalimbali na lengo la Serikali ni kuhakikisha tunaunganisha kwa barabara za lami Miko na Wilaya zetu zote nchini," amesema.

**Miradi mingine inayoendelea kujengwa ipo katika hatua mbalimbali na lengo la Serikali ni kuhakikisha tunaunganisha kwa barabara za lami Miko na...**

Katika kuboresha miundo mbinu hiyo, Rais pia amefungua daraja la msingi pamoja na Barabara za maingilio za lami zenye urefu wa kilomita moja Wilayani Mkalama mkoani Singida.

Daraja hilo ni kiungo muhimu kwenye shughuli za uchumi, usafiri na usafirishaji katika mkoa ya Singida na Mikoa Jirani ya Simiyu, Mwanza, Mara, Manyara,

>> INAENDELEA UK. 13

Siasa

# Rais Samia aziunganisha Mbeya, Singida kwa lami



>> INATOKA UK. 12

Arusha pamoja na maeneo mengine ya nchi.

Akizungumza na wananchi wilayani Mkalama Rais Samia amesema daraja hilo lenye urefu wa mita 100 ni kiungo muhimu kati ya ukanda wa kati na nchi za Afrika Mashariki hususani kwenye mpaka wa Sirari Mkoani Mara kupitia mkoa wa Simiyu.

Amesema ana amini uwepo wa daraja hilo na madaraja mengine yote yaliyojengwa katika mkoa huo yatachochea zaidi biashara ya mazao ya Kilimo, Ufugaji pamoja na bidhaa kutoka katika viwanda vidogo vidogo.

"Wito wangu kwenu ni kufanya kazi kwa bidii ili muweze kuona manufaa ya uwepo wa daraja hilo, muhimu zaidi tutunze miundombinu ya madaraja yote yaliyojengwa ili yaweze kutufaa leo na huko tunakokwenda'.

"Madaraja haya yanajengwa kwa gharama kubwa kama mlivyosikia hapa jumla ya shilingi bilioni 11 na milioni 208 zimetumika kwenye ujenzi wa daraja hili la msingi tunaloliona hapa, uzuri zaidi ni kwamba limeshawekewa taa tayari kwa maana hiyo kuna uwezekano kabisa tukitoka kufunga ndoa zetu huko tukaomba ruhusa ya kufunga maua hapo tukapiga picha zetu za ukumbusho," amesema.

Kwa upande wake Waziri wa Ujenzi Innocent Bashungwa amesema daraja hilo la msingi linaenda kuungana na daraja la Sibiti ambalo linaunganisha wilaya za Meatu upande wa Simiyu na Wilaya ya Mkalama Mkoani Singida.

"Kwa maelekezo yako Mheshimiwa Rais kwamba madaraja yote haya mawili tuweke taa kwa ajili ya usalama, hapa kwenye daraja la Msingi tumeshatekeleza agizo lako taa tumeshaweka na upande wa daraja la Sibiti agizo lako tunaendelea kulitekeleza."

Serikali pia imefanya ujenzi wa daraja kubwa la Itembe lenye urefu wa mita 150 pamoja na mradi kabambe wa kuunganisha Mikoa ya kanda ya ziwa, kanda ya kati na Kaskazini kuanzia Karatu mpaka Mbulu – Hydom – Singida mpaka daraja la Sibiti kuelekea Simiyu yenye urefu wa Kilomita 389.



Akizungumza na Wananchi mkoani Singida Waziri Bashungwa amesema barabara hiyo inayojengwa kwa kiwango cha lami kwa kutumia utaratibu wa Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC +F) kwa upande wa mkoa wa Singida wana kilomita 78.

Amesema wizara yake kupitia TANROADS inandaa nyaraka na kuomba kibali kwa ajili ya kutangaza tenda ya ujenzi wa barabara ya lami kilomita 10 Nduguti Makao Makuu ya Wilaya ya Mkalama.

Amesema upembuzi yakinifu umekwishafanyika katika barabara za lami za kilomita 11.5 Ilongelo makao makuu ya Halmashauri ya Singida; na kwamba barabara ya kuanzia Iguguno – Nduguti – Gumanga hadi Mkalama wenye kilomita 89 ambapoio serikali imeweka kipaumbele ili iweze kuwasaidia wananchi kwenye shughuli za usafiri na usafirishaji katika Wilaya ya Mkalama na Wilaya Jirani kuelekea Dodoma.

"Daraja la msingi ambalo limekamilika linaenda kuungana na daraja la Sibiti (ambalo limekam ilika) linalounganisha wilaya ya Meatu upande wa Simiyu na Mkalama Singida; Mhe Rais ulitoa maelekezo kwamba barabara ambazo zinaingia daraja la Sibiti upande wa Meatu, umetoa fedha tunajenga kilomita 5 na Mkalama ulituelekeza tujenge kilomita 20 tayari Mkandarasi yupo eneo la mradi," ameongeza.

Daraja hilo lililozinduliwa ni sehemu ya barabara inayoanzia Ulemo inaenda Nzega, Gumanga hadi Nyahaha yenye urefu wa kilomita 62 pamoja na kilomita 1 ambayo imejengwa kuzunguka daraja hili.

"Rais ulishatoa fedha kilomita saba za lami zilijengwa na kufanya ziwe jumla ya kilomita 8nane, pia umetoa fedha mkandarasi yupo eneo la mradi ujenzi wa daraja kubwa la Itembe unaendelea," amesema Waziri Bashungwa.

Awali Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Mohamed Besta amesema mtandao wa barabara hii unaanzia Mbeya Mjini kwenda Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kaskazini ambapo ikifika Rungwa karibu na Hifadhi ya Taifa ya Wanyama ya Rungwa inagawanyika mara mbili kwenda Shinyanga na Katavi kupitia barabara ya Rungwa – Ipole (kilometa 174.14) na kwenda Singida kupitia barabara ya Rungwa – Itigi – Mkiwa (kilometa 212.79). Mhandisi Besta amesema barabara hiyo ni muhimu kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kwa Taifa na nchi jirani wa Zambia, Malawi, Uganda, Burundi na Kenya.

"Hii ndio njia fupi ya kuunganisha mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kaskazini. Kwa ajili ya utekelezaji barabara ya Makongolosi ambapo gharama zote za ujenzi zimelipwa na serikali ya Tanzania," amesema.




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

**Kanda ya Kaskazini ambapo ikifika Rungwa karibu na Hifadhi ya Taifa ya Wanyama ya Rungwa inagawanyika mara mbili kwenda Shinyanga na Katavi kupitia barabara ya...**

Utalii



# Maisha, maajabu na uwezo wa mnyama nungunungu

**Na Godfrey Sanga kwa Msaada wa Mitandao**

NUNGUNUNGU au nungu, ni wanyama wagugunaji wenye ngozi iliyotawaliwa na miiba iliyochongoka wanayoitumia kama moja ya kinga dhidi ya maadui.

Walitajwa kuoneakana kwa wingi na rahisi miaka mingi iliyopita.

Pia wanashika nafasi ya tatu katika wanyama wagugunaji kwa ukubwa, wakitanguliwa na capybara na buku.

Nungu wana urefu kati ya sentimita 20 na 25. Uzito wao ni kati ya kilo 5.4 na 16.

Wana umbo la duara, wakubwa na wataratibu. Nungunungu huwa katika rangi mbalimbali ya kijivu na mara chache nyeupe.

Hujihami kwa miiba pia hukaribiana kufanana na kule kwa kalunguyeye (Erinaceomorpha) na ekidna (Monotremata).

**SPISHI**

Nungu ni miongoni mwa spishi 29 za wanyama wagugunaji (rodent) wa familia ya Erethizontidae au Hystricidae. Nungu wanatofautiana kwa ukubwa.

Nungu aitwaye Rothschild's Porcupine wa Amerika ya Kusini ana uzito pungufu ya kilo moja ukifananisha na wa Afrika.

Anaweza kukua mpaka kufikia kilo 10. Familia mbili hizi za nungu ni tofauti kabisa ingawa wote wapo kwenye tawi la Hystricognathi wa oda ya Rodentia, hawahusiani sana. Inaaminika kuwa wametokana na hystricognaths wengine takribani miaka milioni 30 iliyopita.

Nungu wa miaka ya leo, wana umbo dogo kwa kawaida huku miiba yao ikiwa imejishikiza mmoja mmoja badala ya makundi, pia hutajwa kuwa wakweaji wazuri, na hutumia muda wao mwingi juu ya miti.

**UMRI**

Nungu kwa wastani wana uwezo wa kuishi muda mrefu na wanashikilia rekodi miongoni mwa familia yao ya rodent kwa kuishi kwa kiasi cha muda mrefu zaidi ambayo imevunjwa hivi karibuni na panya aina ya Naked Mole Rat (Heterocephalus glaber).

**MIIBA**

Miiba ya nungu huchukua sura mbalimbali kulingana na spishi, lakini yote ni nywele zilizoboreshwa na kufunikwa na keratini, na zimejishikiza kwenye misuli ya ngozi.

Nungu wa kale (Hystricidae), wana miiba iliyojikusanya kwenye makundi huku kwa nungu wa miaka leo (Erethizontidae), miiba mmoja mmoja, imechanganyika na ufumwele yaani manyoya ya chini na nywele.

Miiba huachiwa kwa kuigusa au hudondoka pale ambapo nungu anajitikisa, lakini hawezi kamwe kurushwa kwa adui, pamoja na imani iliyozoeleka.

Miiba mipya hukua huchukua nafasi ya ile iliyopotea.

Mwiba huanza kuwa mwembamba na kujipinda unapokaribia kushikana na ngozi. Ndiyo sababu nungunungu hawezi kuchomwa na miiba yake hata akianguka kutoka mahali palipoinuka.

**MAKAZI**

Nungu hupatikana sana katika maeneo ya kawaida na tropiki ya Italia, Afrika na Amerika ya Kusini na Kaskazini.

Nungu huishi kwenye misitu, jangwani sehemu zenye miamba, vilima na nyikani. Baadhi ya nungu wa miaka ya leo huishi kwenye miti, lakini nungu wa miaka milioni zaidi iliyopita, waliependelea zaidi ardhini.

Nungu hupatikana hata kwenye miamba katika ardhi yenye urefu wa mita hata zaidi ya 3,700. Nungu ni wanyama wanaopenda kuonekana au kujitokeza usiku zaidi.

> **Nungu hupatikana hata kwenye miamba katika ardhi yenye urefu wa mita hata zaidi ya 3,700. Nungu ni wanyama wanaopenda kuonekana...**

Majira ya baridi kali, nungu hutumia muda mwingi akiwa amelala, ana tezi maalum inayomsaidia kusawazisha joto la mwili wake, majira haya hula kwa nadra sana hivyo hutumia mafuta ya ziada anayohifadhi mwilini mwake.

Ukijaribu kumfuga nungunungu, hupanda ukutani au kwenye bomba la maji na kuponyoka kwani anapenda kuishi katika eneo kubwa.

Na hii, diyo sababu, si rahisi kumfuga au kumfanya awe mnyama kipenzi, Ni vizuri zaidi kwamba hafugwi kwa kuwa yeye hubeba viroboto wengi sana siku zote.

**ULAJI**

Nungu hupendelea zaidi chumvi, anapotafuta chumvi wakati mwingine wanaweza kufika mpaka makazi ya watu na hupendelea kukaa kwenye mbao zilizopakwa sodium naitreti, rangi za kuta, mishikio ya vifaa, viatu, nguo na vitu vingine vilivyopata jasho.

Nungu pia huvutiwa na barabara ambazo chumvi hutumika kuyeyusha barafu, na mara kadhaa huonekana wakilambalamba magurudumu ya gari zilizopita kwenye barabara hizo. Hutumia chumvi maalumu kama moja ya kuwaongezea kinga pindi wanapoumia kupona haraka.

Vyanzo vya asili vya chumvi ambavyo nungu hutumia hujumuisha mimea yenye chumvi chumvi, mifupa ya wanyama, magamba ya miti, matope kwenye udongo wenye chumvi sana, na vitu vilivyoshikwa na mkojo.

**IMANI POTOFU**

Kwa kipindi kirefu, nungu huaminika kuwa na uwezo wa kurusha miiba yao kwa adui, hii imekanushwa vikali, baada ya kufahamu kuwa miiba hulegea na kuanguka yenyewe basi imepunguza hisia za watu kuhusisha na ushirikina. Kwani wengi wao waliamini endapo watakutana na mnyama huyu ni miiba kuanguka, basi kuna hatari ya kifo katika familia yao.

**USILOLIJUA**

Ni vigumu sana kumuona kwa vile anaishi kwa shaka sana, kwani aonekanapo hushambuliwa na kuuawa kwa ajili ya kutengenezea dawa na kitoweo, wakati mwingine hukamatwa na kufugwa.

Anaposhtuliwa, nungunungu hujikinga kwa kujikunja kama mpira, Misuli yake yenye nguvu hukaza ngozi yake yenye miiba na kuufunika mwili mzima, Ngozi hiyo yenye miiba hufunika kichwa, mkia, miguu na sehemu zake za chini na anaweza kujikunja hivyo kwa muda mrefu.

Nungunungu huhisi njaa wakati wa jioni. Chakula chake cha jioni huwa wadudu na minyoo, lakini wakati mwingine anaweza kula panya, chura, mjusi au hata njugu na baadhi ya matunda.

Uchambuzi

# Tufanye haya "tunapojitafuta" kuachana na mkaa na kuni



**Aliyekuwa Meneja Mradi wa Kuleta Maguzi ya Mkaa Tanzania (Mkaa Endelevu) kutoka Shirika la Kuhifadhi Misitu Asilia Tanzania, (TFCG), Charles Leonard akitoa maelezo kwa wananchi na kamati ya Siasa ya CCM, Wilaya ya Kilosa ilipotembelea mradi wa mkaa endelevu katika Kijiji cha Chabima wilayani humo. (Picha ya mtandao).**

**Na Hamisi Kibari**

SERIKALI ilitoa katazo kwa taasisi zote za umma na binafsi nchini zinazoandaa chakula na kulisha watu zaidi ya 100 kwa siku, kusitisha matumizi ya kuni na mkaa ifikapo Januari 31, 2024.

Kwa zile zinazoandaa kwa ajili ya watu zaidi ya 300 kwa siku, zinatakiwa kusitisha ifikapo Januari 31, 2025.

Agizo hilo lilitolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, aliyezihimiza taasisi hizo kutumia nishati mbadala ambayo ni safi kwa ajili ya kupikia.

Kwa kuwa ni lazima watu wale, nishati ya kupikia ambayo sasa taasisi hizo zikiwemo shule na majeshi zinapaswa kutumia ni gesi, umeme, mafuta ya taa, biogas, makaa mawe, mkaa unaotokana na nyasi au takataka, jua, upepo na kadhalika.

Msingi wa agizo hilo unatokana na ukweli kwamba uvunaji holela wa miti kwa ajili ya kupata kuni, mkaa na mbao unachangia katika kuharibu mazingira. Pigia msitari maneno "uvunaji holela" kwani si kila uvunaji wa miti ni holela.

Takwimu za Msingi za Hewa Ukaa (Forest Reference Emission Level-FREL) zilizotolewa mwaka 2016 zilionesha kwamba hekta 469,000 ya misitu hupotea kila mwaka nchini. Hii ni takribani sawa na eneo la mkoa wa Dar es Salaam!

> **Ikaelezwa kwenye semina hiyo kwamba, katika mkatadha huo, ni vyema serikali ikajikita katika uzalishaji wa mkaa kwa njia endelevu, yaani njia...**

Wakati ninajiandaa kuandika haya, nimejaribu kutafuta takwimu mpya ili kujua kama tumepunguza uharibifu huo au umeongezeka lakini sikupata.

Isipokuwa takwimu za Waziri Jafo zilionesha kwamba hekta zinazopotea kwa mwaka ni 46,960, sawa na asilimia 26 ya ardhi. Sina hakika kama alikaririwa vyema au takwimu zangu nilikozichukua ndio kuna shida, lakini la msingi ni kwamba malefu ya hekta za misitu hupotea kila mwaka.

Hatua ya serikali ikitekelezwa itasaidia kupunguza uvunaji holela wa misitu lakini tukumbuke kwamba bado Watanzania walio wengi wataendelea kutumia kuni na mkaa kwa kupikia.

Takwimu zilizowahi kutolewa kwenye semina moja niliyoshiriki mwaka juzi zilionesha kwamba kati ya Watanzania 100, ni wanne tu waliokuwa wameacha kabisa kutumia mkaa na kuni.

Ikaelezwa kwamba kuni hutumika zaidi vijijini na mkaa mijini, huku karibu asilimia 90 ya mkaa wote unaozalishwa nchini ukitumika katika jiji la Dar es Salaam!

Kwa lugha nyingine, Dar inayofikiriwa kuwa na wakazi wengi wenye kipato cha kati, hawamudu matumizi ya nishati mbadala!

Katika warsha moja niliyoshiriki mjini Morogoro, ilielezwa kwamba ingawa sera zilizopo zinajielekeza kwenye hizo nishati mbadala, bado bidhaa hizo ni ghali kwa Watanzania walio wengi na pengine ukawa pia mzigo kwa taasisi zinazotakiwa kuachana na mkaa!

Ikaelezwa kwenye semina hiyo kwamba, katika mkatadha huo, ni vyema serikali ikajikita katika uzalishaji wa mkaa kwa njia endelevu, yaani njia isiyoumiza misitu.

Kuna njia ya namna hiyo? Ndiyo. Akiwasilisha mada kwenye warsha niliyoshiriki kuhusu 'Umuhimu na Manufaa ya Kuwa na Mpango wa Uvunaji wa Mkaa na Mbao Endelevu', aliyekuwa Meneja wa Mradi wa Kuleta Mageuzi ya Uzalishaji Mkaa Tanzania (TTCS), Charles Leonard, alisema hatua ya kuuona mkaa kama janga badala ya kuugeuza fursa ni kukimbia ukweli.

Warsha hiyo ilikusanya maofisa kutoka halmashauri mbalimbali za miji na wilaya nchini pamoja na kutoka kwenye idara mbalimbali za serikali. Baadhi ya maofisa misitu, mipango, kilimo na mazingira waliohudhuria warsha hiyo walitoka katika halmashauri za Kilwa, Kilindi, Kilosa, Tabora, Handeni, Kilolo, Kigoma na kadhalika.

Leonard kutoka shirika lisilo la Kiserikali la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), alisema kwamba kupitia takwimu zilizopo ikiwemo ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) 2013, mchango wa sekta ya mkaa kwenye uchumi wa nchi ni takribani Sh trilioni 2.2, kiwango ambacho hakuna zao lolote kubwa la biashara linalozalishwa nchini linakifikia!

Hata hivyo, alisema kwamba faida inayopotea kwa mwaka kutokana na uzalishaji holela wa mkaa ni Sh bilioni 220.

"Tuna takribani miaka 20 ya kuendelea kutegemea mkaa. Kama hali ndiyo hiyo, hatuwezi kukaa kimya badala ya kuja na

>> INAENDELEA UK. 16

Uchambuzi

# Tufanye haya "tunapojitafuta" kuachana na mkaa na kuni

>> INATOKA UK. 15

mpango mkakati wa uzalishaji mkaa endelevu ambao utatupatia mkaa, serikali ikipata pia mapato yake stahili na bado tukalinda misitu na mazingira kwa ujumla," alisema.

Alisema ni katika muktadha huo, TFCG kwa kushirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) walianzisha mradi wa TTCS katika vijiji takribani 30 nchini ambao viongozi wetu, akina Jafo wanapaswa kuitembelea kuona kama wanaweza kujifunza kitu.

Je, ni kweli, kuna mkaa endelevu? Jibu ni ndiyo. Mimi nimeshuhudia. Mradi huo huanza kwa kijiji kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi, kisha eneo la asilimia 10 mpaka 15 la msitu wa kijiji ndilo hutengwa kwa ajili ya uzalishaji mkaa miaka yote na maeneo mengine hutengwa kwa ajili ya shughuli nyingine. Mkaa huzalishwa kitalaamu kwa kuruhusu miti kukua na kuzaliana upya na hivyo uzalishaji kuwa endelevu.

Katika eneo hilo la asilimia 10 mpaka 15, kunatengwa vitalu vya mita 50 kwa 50 vinavyovunwa kwa kurukwa. Kama kitalu A kinavunwa leo, B kinarukwa hadi C na Bikitarejewa baada ya miaka 12 katika mzunguko wa miaka 24 ambapo kitalu kilichovunwa leo huwa kimerejea kuwa msitu. Miti yenye sifa tu ndio inayovunwa kwa ajili ya mkaa. Miti inayofaa kwa mbao inaachwa au iliyo katika vyanzo vya maji pia haiguswi.

Vijiji vimenufaikaje na mpango wa mkaa endelevu? Katika wasilisho lake, Leonard alisema tangu mradi huo uanze mwaka 2012, zaidi ya shilingi bilioni moja zimeshakusanywa huku uharibifu wa misitu ukikoma kwa asilimia kubwa katika vijiji vinavyoendesha mradi huo.

Siku alipotembelea mradi kama huo katika kijiji cha Kitunduweta kilichoko katika tarafa ya Ulaya, aliyekuwa mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Adamu Mgoyi alisema:

"Ni nadra sana kukuta wananchi wanaposikia wametembelewa na ujumbe kama huu, wao ndio wakawa waelezaji wa miradi yao ya maendeleo. Kwa kawaida huwa ni hali ya viongozi kupokea kero na malalamiko kutoka kwa wanakijiji."

Katika risala yao iliyosomwa na aliyekuwa Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Margaret Magele (sina hakika kama bado yupo), alisema mradi wa kuzalisha mkaa endelevu umechangia katika kukiwezesha kijiji kujenga ofisi ya kisasa, kukarabati madarasa mawili na ujenzi wa nyumba ya mwalimu.

Lakini faida kubwa alisema ni utanzaji wa misitu baada ya wananchi kuona faida wanayopata kutokana na msitu wa kijiji ambao awali kabla nya mradi waliiona haina mwenyewe!

Tukirudi kwenye warsha, Leonard katika wasilisho lake alisema moja ya changamoto iliyopo ni kukosekana kwa sera inayozungumzia umuhimu wa kuwa na uzalishaji endelevu wa mkaa nchini.

Akijibu hoja hiyo, Ofisa Misitu Mkuu, kutoka Idara ya Misitu na Nyuki, Wizara ya Maliasili na Utalii, Ludovick Uronu (sijui pia wasifu wake wa sasa), alisema sera mpya ya misitu inayoandaliwa sasa imegusia suala zima la uzalishaji mkaa endelevu.

Je, hoja yangu ya msingi ni ipi hasa? Kuna nukta mbili tatu ninazoziangalia. Kwanza, tamko la Waziri ni zuri kwa sababu, licha ya kulinda mazingira, upishi wa mkaa na kuni ni mgumu kulinganisha na wa nishati nyingine mbadala. Taasisi hizi zinapaswa kuanza kutumia nishati mbadala lakini pia zingeruhusiwa

**Kimsingi, asilimia 70 mpaka 80 ya matukio yanayosababisha upotevu wa misitu nchini ni ufyekaji wa misitu kwa ajili ya upanuzi wa mashamba na kilimo cha kuhamahama.**

kutumia mkaa uliozalishwa kwa njia endelevu pekee na kuachana na unaozalishwa holela ambao ndio mwingi sokoni. Wafungwa wanaweza kusaidia katika hilo.

Lakini maswali ya kujiuliza. Je, hatua ya hizo taasisi kutumia nishati mbadala itasaidia kupunguza uzalishaji holela wa mkaa na kuni nchini? Ni lini agizo kama hilo litashuka hadi kwa wananchi wa kawaida? Je, nishati mbadala zilizopo zitatuondoa kabisa kwenye haja ya kutegemea mkaa na kuni?

Kuhusu nishati mbadala, je, gharama ya mitungi ya gesi itashuka kuwawezesha Watanzania wengi kumudu?

Kulikuwa na mpango wa kusambaza mabomba ya gesi asilia kwenye taasisi na nyumba mbalimbali kwani gesi hiyo, tofauti na hii ya mitungi, gharama zake ziko chini.

Hili limefikia wapi? Je, bei ya umeme nayo itapungua kidogo ili sasa taasisi na watu watumie zaidi majiko ya umeme yaliyoondolewa ushuru na kuwa rahisi kuyanunua?

Tuliwahi kuambiwa kwamba, umeme kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere ukianza, gharama zitapungua. Hilo litatekelezwa kiasi cha kuwawezeha sasa watanzania hadi vijijini kumudu kutumia majiko ya umeme?

Katika kujijibu baadhi ya maswali hayo, mimi naona kwamba licha ya hatua hiyo kusaidia kupunguza matumizi ya mkaa, itakuwa ni kwa kiwango kidogo sana.

Kwa sasa, tulipaswa kama nchi kutumia nguvu kubwa kujikuta kwenye uzalishaji wa mkaa kwa njia endelevu kuliko hata hayo makatazo.

Kwa kuwa kuna vijiji zaidi ya 30 vilivyokuwa vinaendesha mradi wa mkaa endelevu serikali inapaswa kwenda kujifunza kwenye vijiji hivi na kuanzisha miradi ya mkaa endelevu katika kipindi hiki 'tunachojitafuta' kugeukia nishati mbadala.

Hii ni kwa sababu kwenye vijiji hivi hakuna uvunaji holela wa miti. Mkaa unaozalishwa huko ni endelevu na hili likitekelezwa

Tanzania nzima lina manufaa makubwa. Natamani wakubwa kama Waziri Mkuu, Makamu wa Rais au Rais mwenyewe wafike kwen ye vijiji hivi katika wilaya za Morogoro, Kilosa, Mvomero na kadhalika na kuona mbinu ya uzalishaji mkaa na kuni kwa njia endelevu isivyoharibu misitu ili kusambaza mbinu hii nchi nzima.

Nukta nyingine ninayotaka kusema ni kwamba, ingawa ni kweli mkaa na kuni vinachangia uharibifu wa mazingira, lakini ni kwa asilimia saba tu kwa mujibu wa tafitizilizopo. Hii ni kinyume kabisa na jinsi wengi wanavyofikiri.

Kimsingi, asilimia 70 mpaka 80 ya matukio yanayosababisha upotevu wa misitu nchini ni ufyekaji wa misitu kwa ajili ya upanuzi wa mashamba na kilimo cha kuhamahama. Watetezi wa misitu wamekuwa wakihimiza nchi kujikita katika kilimo hifadhi, yaani kilimo cha kisasa kinachotumia eneo dogo kwa mavuno mengi. Hili nalo linapaswa kukazaniwa na ofisi ya Jafo pamoja na kudhibiti kilimo cha kuhamahama.

Asilimia zinazobaki katika kumaliza misitu nchini zinachukuliwa na matukio ya kuchoma moto misitu na shughuli za ufugaji. Siku hizi ukienda kwenye misitu ya wilaya kama za Kilwa, Ruangwa na Liwale mkoani Lindi kuna makundi ya kutisha ya ng'ombe. Mimi ninayeandika haya sijahadithiwa na mtu bali nimeona mwenyewe.

Wakati mazingira hayajawa mazuri ya kuachana kabisa na mkaa na kuni, uzalishaji endelevu wa mkaa na kuni ni jambo la kuzingatiwa sana kufanywa na serikali kupitia halmashauri zetu kwa sababu una faida lukuki. Maeneo ya kujifunza yapo.





Paul Mng'ong'o

## KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Nguzo tano za kuzingatia kwenye maisha

KAMA ukiyapa nafasi ya pekee na kipaumbele mambo haya matano tunayoyataja leo kwenye jukwaa hili bila shaka yatakuwa ya baraka na amani katikia maisha yako.

Mosi, fanya maamuzi ya dhati yatakayoboresha afya yako (healthy), jambo la pili ni kufanya bidii ya dhati kukuza uchumi wako (personal finances), tatu jenga maarifa na ujuzi kila siku (knowledge and skills), jambo la nne, hakikisha unatumia sana hekima (wisdom) na jambo la tano ni kuhakikisha unampenda na kumtegemea Mwenyezi Mungu.

**KUFANYA MAMBO KWA KUZINGATIA AFYA**

Afya ndiyo mtaji wa maisha yako. Bila afya mambo yako muda si mrefu yatasimama kutokana na matatizo ya kiafya. Badala ya wewe na afya kutafuta pesa, utaanza kazi ya wewe na pesa kutafuta afya! Mambo ya msingi kuhusu afya ni ulaji sahihi, kuwa na mtazamo sahihi, kufanya mazoezi na kujipa muda wa kupumzika: -

**Ulaji sahihi**

Ni vizuri kula vyakula vyenye virutubisho sahihi na kuepuka sumu mbalimbali. Vitu vikubwa vya kuepuka kwenye ulaji wetu ni: -

- Matumizi makubwa ya wanga mwilini
- Matumizi makubwa ya mafuta. (yanayoganda na yasiyoganda)
- Matumizi makubwa ya sukari.
- Matumizi ya dawa yasiyo na ushauri wa wataalamu.
- Kuzingatia unywaji wa maji ya kutosha

Watalaamu wa lishe wanasema kwamba Watanzania wengi hawana shida ya protini inayopatikana kwenye vyakula kama nyama, samaki, maharage, maziwa na mayai. Wala miili yao haina upungufu wa wanga unaopatikana kwenye ugali, ubwabwa, maandazi, chapati, mihogo, viazi na kadhalika.

Tatizo kubwa la Watanzania ni upungufu wa vitamini (A, B, C, D nk) na madini kama ya chuma, kalsiamu, fosforas, potasiamu (magadi), sodiamu nk. Viti hivi; madini na vitamini hupatikana zaidi kwenye mbogamboga na matunda.

**Mtazamo sahihi**

Mtazamo sahihi ni mtazamo chanya. Ni vizuri ujifunze kufikiri kwa mtazamo chanya na kuachana na fikra zinazokuletea maumivu na msongo wa mawazo.

**Kufanya mazoezi**

Mazoezi ya mara kwa mara ni jambo muhimu linaloimarisha afya.

Kutokana na mtindo wa maisha wa watu wengi katika zama hizi, inashauriwa kufanya mazoezi angalau dakika 30 kwa siku na angalau mara tatu kwa wiki.

Kupumzika

Unapaswa kupata muda mzuri na wa kutosha wa kupumzika. Hii ni pamoja na kupata muda wa kutosha wa kulala.

**MAFANIKIO KIUCHUMI**

Mafanikio ya kiuchumi ni zao la uamuzi madhubuti wa kuishi kwa kufuata misingi na kanuni sahihi za kiuchumi. Hakuna njia ya mkato zaidi ya hii.

Kuna misingi na kanuni kubwa nne za mafanikio kwenye maisha: -

**Uamuzi thabiti (Determination**

Njia za mafanikio ni ngumu na mara nyingi zinavunja moyo na kukatisha tamaa. Njia hizi zinahitaji kujikana na kuachana na mambo mengine, hivyo si kitu rahisi.

**Mpango thabiti (A clear Plan)**

Ili kufanikiwa lazima uwe mtu wa kupanga mambo yako na kuyasimamia sawasawa.

-Panga kila kitu, mfano, Panga vizuri jambo/mambo ya kufanya (what to do)

-Tambua malengo ya msingi ya jambo husika (target)

-Panga rasilimali zako na mgawanyiko wake (capital)

-Tambua na upange mahitaji ili kufanikisha (requirements)

-Panga wahusika wa jambo kwa sifa na uwezo wao (proper HR)

-Weka vipaumbele (prioritize)

-Panga matumizi sahihi ya muda (time Management)

-Panga muda unaokusudiwa (time Frame)

-Gawanya muda kwenye vipindi vya tathmini (evaluation Periods)

-Panga viashiria vya matokeo kusudiwa (Project KPIs)

-Tambua maeneo ya uwezekano wa kushindwa na uyapangie mbinu za suluhu (Worst case scenarios and the mitigation factors) "Plan B?"

NK

**Jitihada (Hardworking)**

Mafanikio bila kufanya kazi kwa juhudi, ni sawa na kuyaimba tu mafanikio na kamwe mafanikio halisi hayatatokea.

Mtandao (Network) itakayokusaidia

Ili kufanikiwa kiuchumi lazima uwe na mtandao (uzungukwe) na watu sahihi watakaokusaidia kukua.

**Bahati/Fursa**

Pamoja na yote, njia ya mafanikio inahitaji bahati kwa lugha ya kijamii au fursa kwa lugha ya kiuchumi. Hapa tunaongelea mambo makubwa matatu:

-Upate fursa,

-Uzione fursa, na

-Uzitumie fursa kwa usahihi.

**MAARIFA NA UJUZI (KNOWLEDGE AND SKILLS)**

Maarifa na ujuzi ni maelezo ya kinadharia na ya vitendo, ukweli au ujuzi ambao tunapata kupitia uzoefu au kwa kujifunza. Maarifa yetu yanaongezeka tunapopata uzoefu zaidi. Ujuzi uliokuzwa vizuri unaweza kutufanya kuwa wataalamu katika uwanja fulani. Ujuzi unaweza kujifunza pia.

**HEKIMA (WISDOM)**

Hekima ni zao la matumizi ya mjumuiko wa elimu sahihi, ufahamu mzuri, ujuzi, maarifa na uzoefu kwenye kutazama na kutathmini mambo. Mtu anayefikiria kwanza kabla ya kusema au kutenda na akatenda sawasawa, huyo anahesabika kuwa mwenye hekima.

Kuna watu wengi wanapata hali hii kutokana na vyanzo mbalimbali kama vile: -

-Mazingira aliyokulia (environmental affection)

-Watu wanaomzunguka (mob psychology),

-Miongozo au misingi anayoiamini (values)

-Kutembea maeneo mengi (exposure)

-Mambo mengi aliyoona au kukutana nayo (experience)

-Elimu na uelewa (set of rules)

Hekima ndiyo ulinzi wa mafanikio tunayokuwa tumeyajenga. Matatizo mengi kwenye maisha ni matokeo ya kufanya maamuzi bila ya kutumia hekima.

**KUMTEGEMEA MUNGU**

Siri kubwa ya watu waliofanikiwa na wengi kuwa imara (thabiti) kwenye maeneo yao, siri ambayo haitajwi sana ni kumtegemea na kumcha Mungu wao (kuwa na hofu ya Mungu).

Maisha bila Mungu ni maisha ya utupu yasiyo na mwelekeo. Ni maisha ya kufanya hata mambo ya hovyo bila kuwa na hofu yoyote.

**HITIMISHO:**

Hakuna uhaba wa maarifa kwenye zama tunazoishi sasa, maarifa yapo tele na yanapatikana kwa urahisi kabisa. Unaweza kujua chochote unachotaka kujua.

Kinachokosekana ni juhudi zako katika kupata maarifa sahihi na kuyafanyia kazi.

Kama ungependa kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (Unaweza kuwa taasisi binafsi au ya serikali, kikundi cha kijamii, kanisa, umoja, NGO, mtu binafsi n.k) basi karibu sana, nitashirikiana nawe kwa neema na msaada wa Mungu.

Karibu tuwasiliane kwa namba 0676055444 au barua pepe mngongopaul@yahoo.com na kwenye mitandao ya kijamii.

**Paul Mng'ong'o**
**Your Partner in Growth.**





Na Hamisi Kibari

Mtanzania wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 5

**Chris, anajikuta akinogewa na penzi la Joyce, Miss Tabora wa zamani. Mahusiano hayo yanamfanya ajifunze kunywa pombe na kutelekeza kabisa familia. Mkewe anaamua kwenda kwao kulalamika. Hatua hiyo inamfanya Chris ahamie nyumbani kwake na hawara yake huyo Joyce ili kupunguza gharama za kuishi hotelini. Dada yake anamjia juu kwa kitendo hicho akimshauri akampangie chumba hawara yake lakini Chris anakataa. Sasa mkewe, Mama Kenny amerejea ghafla na kumkuta Chris na Joyce wakiwa sebuleni. Nini kitatokea?**

Kabla hata ya kukaribishwa, mlango ukafunguliwa. Mama Kenny akaingia akiwa ameandamana na mwanawe mdogo, Huba.

Alikuwa pia ameandamana na kijana mmoja ambaye alimsaidia kuingiza ndani kapu la vyakula pamoja na begi lake. Mama Kenny alimlipa ujira wake huyo kijana pale mlangoni. Akaingia na kujikuta anasimama katikati ya sebule kwa mshangao.

Alikuwa anawashangaa watu walioketi kwenye meza ya chakula, Chris na Joyce ambao pia walibaki wakimwangalia mama Kenny kwa mshangao.

"We mwanamke vipi? Unakujaje bila taarifa?"

"Taarifa ipi. Mtu anaporudi kwake anahitaji kutoa taarifa."

"Kwa hiyo wewe umekuwa ni mtu wa kuondoka bila taarifa na kurejea nyumbani bila taarifa, siyo?"

"Hata kabla sijaondoka, lini umepokea simu yangu. Nitatoa taarifa kwa mtu ambaye hapokei simu?" Akahoji Mama Kenny. Mwanawe Huba aliyekuwa amesimama pembeni mwake alimsalimia baba yake. Chris hakujibu.

Mama Kenny akamwambia Huba aketi kwenye kochi kisha akaanza kupiga hatua kuelekea chumbani kwake.

"Wewe unakwenda wapi huko?" Alihoji Chris.

"Yaani hujui nakwenda wapi?" Ninawapisha na mambo yenu. Nakwenda chumbani kwangu."

"We subiri. Njoo kwanza hapa."

Mama Kenny hakujibu bali aliendelea na safari ya kwenda chumbani kwa sababu mlango wa chumba ulikuwa wazi huku taa ikiwaka kwa ndani.

Chris alimwendea mama Kenny haraka na kwa hasira na kumkwida wakati akitaka kutambuka kizingiti cha cha kuingia chumbani kwake. Chris akamvuta kwa nguvu kutoka nje.

"Mwanamume mshenzi sana. Mshenzi sijawahi kuona... Unawezaje kuniletea hawara ndani kwangu halafu unanizuia kuingia chumbani kwangu. Yaani hujui miye ni mke wa ndoa na hapa ni kwangu?"

"Unaniita mshenzi."

"Mshenzi kabisa, na kwa mtu kama wewe, na hilo neno lina unafuu, natafuta neno zito zaidi ya hilo sijapata," alisema Mama Kenny kwa hasira.

"Nitakuharibu sura sasa hivi... Hivi wewe mwanamke umeshindwa kujua kwamba hunifai na sikutaki. Nini kimekuleta kuharibu starehe za watu. Hebu toka nje."

"Nitoke niende wapi... Kama hun'taki hilo ni suala jingine. Hapa ni kwangu. Wazazi wangu wanakuja keshokutwa tuongee haya mambo. Hapo ndipo nitajua kuondoka kama kweli hunitaki. Kwetu sijafukuzwa. Nilitokea mlangoni, sikupitia dirishani miye," alijibu Mama Kenny kwa kujiamini.

"We mwanamke. Si ulikwenda kwenu, sasa imekuwaje umerudi bila kuitwa? Nasema lazima utoke nje."

"Sikuelewi na wala sitoki. Nitoke niende wapi. Kwa sababu ya hicho kinyago chako?"

Joyce alinyanyuka kwa hasira kusikia kaitwa kinyago: "Nani unamwita kinyago?"

"Wewe mkosa adabu na mwizi wa waume za watu. Koma kabisa kuninyooshea kidole... Mbwa kasoro mkia."

Joyce alimgeukia Chris, "Unaona huyu mshenzi anavyonitukana..."

"Koma kuninyooshea kidole wewe kinyago. Nitakuzaba vibao mshenzi mkubwa," alisema Mama Kenny na Joyce akaanza safari ya hasira kwenda kukamatana na Mama Kenny.

Chris alitoka kwa Mama Kenny na ili kumzuia Joyce ambaye alikuwa anakuja kwa kasi kumvaa Mama Kenny.

"Thubutu, jaribu nikuharibu sura swine mkubwa... Mbwa kasoro mkia."

Joyce alizidi kukasirika. Akafanikiwa kumtoka Chris na kwenda kumvaa Mama Kenny. Mama Kenny akamwahi Joyce na kumtupa chini. Chris alikasirika na kuingilia kati. Akamvamia Mama Kenny na kuanza kumpiga. Mama Kenny alianguka chini. Chris akaendelea kumpiga ngumi na mateke pake chini kwa hasira. Mtoto Huba akawa anamlilia mama yake. Chriss akazidi kumpiga kwa hasira mateke mfululizo.

Wakati huo Mama Kenny alikuwa anapiga kelele za kuomba msaada kwamba anakufa. Chriss akazidi kumpiga. Mama Kenny akabaki chini anakoroma na povu likimtoka kinywani.

"Twen'zetu mpenzi, tunachelewa," alisema Joyce.

Chris alimtazama Mama Kenny pale chini kwa hasira. Mtoto wake akawa bado analia pembeni mwa mama yake. Chris hakujali. Akageuka na kumshika mkono Joyce, wakaanza kujongea mlango wa kutoka nje. Walipofika mlangoni, Chriss aligeuka tena kumwangalia mkewe.

"Anajifanya umezirai. Twen' zetu," alisema Chris akisonya.

Alipotoka nje, Chris alikuta watu kadhaa pale nje. Akarudiushia mlango haraka haraka.

"Kuna nini jirani," aliuliza mmoja wao.

"Shwari tu."

"Lakini tumesikia mayowe ya kuomba msaada."

"Kulikuwa na kaugomvi kadogo tu... Unajua tena wanawake. Kila kitu kiko OK," alisema Chris.

* * *

Chris aliwasili nyumbani kwake kwa teksi akiwa amekuja kuchukua baadhi ya vitu vya Joyce ambaye aligoma kwenda kulala nyumbani kwa Chris.

Joyce alisema ni lazima usiku huo alale na vitu vyake ikiwa ni pamoja na vipodozi na nguo zake za kubadilisha asubuhi.

"Sitasubiri cha nini wala nini. Kukicha tu ninarudi hapa kumfukuza huyu mwanamke," alijisemea Chris wakati akishuka kwenye teksi na kumtaka dereva amsubiri kwa dakika zisizozidi tano.

Alishangaa alipogusa mlango kugundua kwamba ulikuwa bado umesindikwa kama alivyouacha. Aliamini wakati wanaondoka kwamba Mama Kenny angeliufunga baada ya kunyanyuka pale alipokuwa amelala.

Alipoingia ndani alishangaa zaidi kuona Mama Kenny akiwa bado amelala palepale sakafuni alipomwacha wakati yeye na Joyce wanaelekea kwenye dansi. Huba pia alikuwa amelala kando ya mama yake. Chris alitaharuki na kuingiwa na woga.

"Nisije nikawa numemuua huyu mwanamke. Hebu ngoja nimwangalie kwa makini. Yaani hajaamka toka muda ule?" Alijisemea woga ukizidi kumvaa.

Chris alisimama akimwangalia Mama Kenny kwa mshangao. Akainama na kumshika mkewe kifuani kuona kama mapigo ya moyo yanafanya kazi. Akamwita huku anamtikisa. Hakuitika. Akamgusa tena kufuani akahisi mapigo yake kwa mbali. Akeweka kidole kwenye pua yake huku kijasho chembamba kikianza kumtoka. Akapata ahueni kidogo baada ya kusikia anapumua.

Alipomuangalia vizuri akagundua kwamba mwanamke huyo alikuwa amejikojolea. Alitoka nje haraka kumwita dereva amsaidie kumbeba mkewe kumpelekea hospitali. Haikuwa hali ya kawaida. Aliwaza kwamba hata kama ni kufa bai ni heri afie hospitali.

Wakati wanaanza kumbeba, yule dereva pia alionekana kushtuka kutokana na hali ya mwanamke huyo.

"Vipi, kawaje. Kafa?" akahoji yule dereva akionesha hofu.

"Ni mzima lakini hajitambui," akajibu Chris huku uso wake bado ukionesha mashaka.

Wakambeba hadi kwenye teksi. Chris akafunga mlango harakaharaka na kurudi kwenye gari.

"Ondoa gari haraka tumwahishe mgonjwa."

"Lakini yule mtoto vipi. Naona umefunga nyumba. Anabaki peke yake au kuna mtu mwingine ndani?"

"Yaani nimechanganyikiwa. Unashaurije. Twende naye?"

"Mtoto mdogo huyo atabakije peke yake. Tumpitishe pale hotelini abaki na yule dada."

"Hapana. Ngoja tumwahishe kwanza mgonjwa. Akishapokelewa nitarudi haraka."

"Hapana. Mambo ya hospitali huwezi kujua yatachukua muda gani. Tukamwache kwa huyo dada. Akiamka hapo halafu asione mtu itakuwa balaa."

Chris alishuka haraka na kwenda kumbeba mwanae Huba. Kisha yule dereva akaondoka kuanza safari ya kwenda hospitali kupitia hotelini alikobaki Joyce.

Walipofika hotelini, Lemon Tree, Chris alishuka harakaharaka akiwa kambeba Huba hadi chumbani alimokuwa amelala Joyce.

Alimweleza kilichotokea na kumtaka abaki na mtoto huyo wakati wanawahi hospitali kumpeleka Mama Kenny ambaye hali yake ilikuwa si nzuru, lakini Joyce alikataa.

"Siwezi kulala na toto la mtu, tena toto la mwanamke anayeniita kinyago, siwezi miye" alisema Joyce akibetua midomo.

"Kuwa na huruma kidogo Joy, tunazidi kuchelewa. Huyu mwanamke anaweza kutufia hapa. Akifa hiyo ni kesi kubwa sana."

"Mpeleke kwa dada yako. Si kaka yake yuko huko. Mpeleke," alizidi kumaka Joyce.



*Itaendelea*

# Israel yashambulia maeneo 400 ya Gaza



JESHI la Ulinzi la Israel (IDF), linasema lilipiga shabaha zaidi ya 400 huko Gaza katika muda wa saa 24 zilizopita, kutoka 320 ilizotangaza katika hatua hiyo hiyo juzi.

Katika taarifa yake iliyotuma kwenye mtandao wake wa X, zamani Twitter, IDF ilisema shabaha zake ni pamoja na wapiganaji wa Hamas waliopanga kurusha roketi kuelekea Israel na shimo la handaki linaloruhusu Hamas kupenya Israel kupitia baharini.

Inasema pia vituo vya amri vilivyotumiwa kuweka silaha kwenye misikiti vilipigwa.

IDF inaongeza kuwa itaendelea kufanya kazi ili kuhakikisha kunakuwa na usalama wa raia wasio na hatia.







## ... Hamas yawachia mateka wawili



Mateka wawili wazee Waisrael walioachiliwa na Hamas juzi ni Nurit Cooper (79) na Yocheved Lifshitz, 85 - - wamewasili Tel Aviv kwa matibabu.

Hamas ilisema iliwaachilia wanawake kwa sababu za "kibinadamu" na kiafya.

Israel imeishukuru Misri kwa usaidizi wake katika upatanishi uliowezesha kuachiliwa kwao na Shirika la Msalaba Mwekundu kwa jukumu muhimu ililofanya kuwarudisha wawili hao nyumbani.

Mume wa Cooper Amiram (85, na mume wa Bi Lifshitz Oded, 83, bado wanazuiliwa na Hamas huko Gaza, kulingana na maafisa wa Israeli.

Nurit Cooper na Yocheved Lifshitz waliwasili kwa helikopta katika hospitali ya Ichilov mjini Tel Aviv

## ... Hezbollah washambuliwa kwa mabomu

Jeshi la Israel limesema lilifanya uvamizi katika eneo la wapiganaji wa Hezbollah nchini Lebanon, kujibu mashambulizi yake ya maroketi kaskazini mwa Israel.

Shambulio hilo lililenga miundombinu ya Hezbollah, ikiwa ni pamoja na mnara na jumba la kijeshi, kwa mujibu wa ujumbe uliotumwa kwenye akaunti ya Jeshi la Israel ya tovuti ya X, zamani ikiitwa Twitter.

Jeshi lilichapisha video inayoonyesha shambulizi la anga kwenye jengo na lilisema lilijibu roketi zilizorushwa kutoka upande wa Lebanon mapema Jumatatu.

BBC haikuthibitisha uhalisi wa video hiyo iliyochapishwa na Jeshi la Israel.

## ...Macron atua Israel, akutana na Netanyahu



**YERUSALEM, Israel**

RAIS wa Ufarans,a Emmanuel Macron, amewasili katika Uwanja wa Ndege wa Ben Gurion nchini Israel, na alitarajiwa kukutana na Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu.

Madhumuni ya ziara hiyo ni kuonyesha mshikamano wa Ufaransa na Israel, kusaidia katika kuachiliwa kwa mateka ambao bado wanashikiliwa na Hamas na kuzuia kuongezeka kwa mzozo wa sasa, washauri wake waliambia Reuters.

Macron pia atakutana na Rais wa Israel, Isaac Herzog, na viongozi wa siasa kali Benny Gantz na Yair Lapid kutoka upinzani wakati wa ziara yake.

BBC.

# Rubani kortini akidaiwa kutaka kuiangusha ndege




**WASHINGTON, Marekani**

RUBANI ambaye hakuwa kazini, ameshtakiwa kwa makosa 83 ya kujaribu kuua baada ya kudaiwa kujaribu kuangusha ndege ya abiria.

Mshukiwa alikuwa ameketi kwenye chumba cha marubani cha ndege ya Alaska Airlines nyuma ya nahodha na afisa wa kwanza kwa mujibu wa taarifa ya shirika la ndege.

Hati ya polisi ilimtaja mshukiwa kua ni Joseph David Emerson, (44).

Ndege hiyo ilikuwa ikitoka Everett, Washington kuelekea San Francisco, California, ikiwa na abiria 80.

Wafanyakazi wa Alaska Airlines Flight 2059, waliripoti tukio hilo kwa udhibiti wa safari za anga.

Katika rekodi ya mawasiliano ya udhibiti wa usafiri wa anga, mmoja wa marubani alisikika akisema: "Tuna mtu ambaye alijaribu kuzima injini nje ya chumba cha rubani," alisema mmoja wa wafanyakazi hao.

Ndege hiyo, inayoendeshwa na Horizon Air, ilipaa saa 11:30 jioni kwa saa za huko na kufika San Francisco saa 1:30 jioni.

Abiria Aubrey Gavello, aliambia ABC News kwamba waliokuwemo hawakujua chochote kilikuwa kibaya na ndege hiyo hadi mhudumu wa ndege hiyo alipotangaza kwamba ndege hiyo ilihitaji kutua mara moja, baadaye akataja dharura ya kiafya.

Abiria mwingine aliliambia kituo hicho kuwa hali hiyo ilishughulikiwa kitaalamu na abiria hawakufahamu kuhusu mgogoro huo.

Katika taarifa, Alaska Airlines ilisema abiria wote waliokuwemo walisafiri kwa ndege baadaye.



# Mayaula Mayoni: Mwanamuziki wa TP OK Jazz aliyetamba AS Vita, Yanga

**Na Daniel Mbega**

**Kuzaliwa:** Novemba 6, 1946
**Mahali:** Leopoldville (Kinshasa), Congo
**Kufariki:** Mei 26, 2010
**Mahali:** Brussels, Ubelgiji
**Klabu alizochezea:** AS Vita Club (Congo DR), Young Africans (Tanzania), Racing Club de Charleroi (Ubelgiji), Racing Club de Jette (Ubelgiji), FC Fribourg (Uswisi), Timu ya Taifa ya Zaire.
Bendi alizopigia: Kundi la Abeti Masikini, T.P. O.K. Jazz na Soukous Stars. Nyimbo alizotunga: Cherie Bondowe I & II, Nabali Mizele, Ousmane Bakayoko, Moni, Ndaya (uliimbwa na M'pongo Love), Nasi Nabali (uliimbwa na Tshala Muana), L'Amour au kilo, Mbongo ebima.

Jina lake halisi ni Freddie Mayaula Mayoni (alizaliwa Novemba 6, 1946 jijini Léopoldville - ambalo sasa linaitwa Kinshasa, katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo) alikuwa mchezaji wa soka na mwanamuziki ambaye tungo zake nyingi bado zingali moto hata sasa zinapopigwa. Maisha yake ya awali Mayaula Mayoni alimaliza shule za awali bila matatizo na kuhitimu alianza elimu ya sekondari mwaka 1962 katika Chuo cha Kisantu.

Tangu akiwa mdogo alipenda sana kandanda. Kati ya mwaka 1968 na 1970 alicheza nafasi ya winga wa kushoto katika timu ya AS Vita Club ya Kinshasa na aliweza kuchaguliwa hata timu ya Taifa ya Congo 'Les Leopards'.

Baba yake alipopata nafasi ya kufanya kazi katika Ubalozi wa Zaire nchini Tanzania, Mayaula alimfuata huku na kujiunga na timu ya Young Africans mwaka huo huo ambapo alikuwa kwenye kikosi kilichotwaa ubingwa kwa mwaka wa tatu mfululizo.

Wachezaji wengine waliokuwa katika kikosi hicho kilichokuwa kinanolewa na Dk. Victor Sanculescu kutoka Romania walikuwa Elias Michael, Kitenge Baraka Said, Boi Idd 'Wickens', Hassan Gobbos 'Wa Morocco', 'Mwamba' Omari Kapera, Gilbert Mahinya, Kitwana Manara, Maulid Dilunga, Juma Bomba, Badi Salehe, Leonard Chitete, Abdulrahiman Juma (nahodha), Freddie Mayaula Mayoni (Zaire) na wengineo.

Itakumbukwa kwamba, Jumamosi Juni 30, 1970 katika mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Karume (kombe hilo lilitolewa na Rais wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Sheikh Abeid Amani Karume), dhidi ya mahasimu wa Yanga, Sunderland (kabla haijaanza kuitwa Simba SC), kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Uwanja wa Uhuru) jijini Dar es Salaam, Mayaula Mayoni alifunga mabao mawili yaliyoipata Yanga ushindi wa 2-1.

Mchezo huo ulishuhudiwa na Rais Karume mwenyewe ambapo Mayaula alifunga mabao yote mawili ndani ya dakika 45 za kwanza, huku lile la Sunderland lilifungwa na Omar Gumbo katika dakika ya 19.

Sunderland sasa ilikuwa inasubiri kulipa kisasi kwenye Ligi ya Mkoa wa Pwani. Yanga ilisawazisha bao hilo kupitia kwa Mayaula mayoni katika dakika ya 32 baada ya kumegewa krosi safi na Maulid Dilunga kabla ya kufumua shuti kali ambalo kipa wa Sunderland, Hassan Mlapakolo, alishindwa kulidaka.

Dakika nne baadaye Mayaula tena akaifungia Yanga bao la pili na la ushindi baada ya kutokea piga-nikupige langoni mwa Sunderland.

Siku hiyo timu zilipangwa hivi: Yanga: Elias Michael, Athumani Kilambo, Boi Idd 'Wickens', Hassan Gobbos, Omari Kapera, Badi Salehe, Leonard Chitete, Abdulrahiman Juma (nahodha),

Kitwana Manara, Maulid Dilunga, Freddie Mayaula Mayoni.

Sunderland: Hassan Mlapakolo, Shaaban Baraza, Mohammed Kajole, Yussuf Salum, Rashid Seif, Omari Gumbo, Ally Kajo, John Kadu (kocha mchezaji), Emmanuel Mbele, Mustafa Choteka, Kimimbi Yusuf Omari.

Mwaka 1971 Mayaula aliondoka Dar es Salaam na kwenda jijini Charleroi, Ubelgiji ili kujiendeleza kimasomo katika kozi ya Data Processing. Huko akajiunga na klabu ya Racing Club de Charleroi kabla ya kujiunga na Racing Club de Jette ya Brussels.

Kwa muda mfupi alichezea klabu ya FC Fribourg ya Uswisi, na ni katika kipindi hicho alipoanza kujifunza kupiga gitaa.

Muda si mrefu akajiunga na bendi ya wanafunzi Wacongo waliokuwa wanasoma Uswisi iliyoitwa Orchestra Africana akiwa anapiga gitaa la rhythm. Aliporudi Kinshasa mwaka 1973, Mayaula akabadili kazi kutoka kwenye mpira na kuwa mwanamuziki mtunzi.

Haikuchukua muda mrefu Mayaula akagunduliwa na Franco Luambo Makiadi aliyemtaka ajiunge na TP OK Jazz, na ndio wakati huo Mayaula Mayoni akatoa kibao cha Cherie Bondowe.

Wimbo huo ulipokelewa vizuri sana na wapenzi wa muziki lakini National Censorship Commission ya Zaire wakati huo, iliupiga marufuku kwa kuwa ulikuwa ni wimbo ambao hadithi yake ilikuwa ni ya kahaba mmoja aliyekuwa akielezea shughuli zake zilivyo, Commission iliona wimbo unatetea ukahaba, hivyo kuupiga marufuku.

TP OK Jazz ililazimika kuusambaza wimbo huo kutokea Ubelgiji na hatimaye ukaenea Congo na sehemu nyingine za Afrika.

Inasemekana kuwa licha ya Franco kumkaribisha OK Jazz, lakini Mayaula Mayoni hakuwahi kuwa mwanachama halisi wa kundi hilo kwani alipendelea kuwa huru kutunga nyimbo zake na kumpa msanii aliyemtaka.

Tungo zake kadhaa zilifanyiwa kazi na TP OK Jazz kama vile Nabali Mizele na Moni. Mwaka 1977 wimbo wake wa Ndaya ulichukuliwa na kuimbwa na mwanamuziki M'pongo Love.

Wimbo huo maarufu ulikuwa unaongea kuhusu mwanamke aliye na furaha kutokana na kuwa na mume bora na kuweza kumdhibiti asitangetange kwa wanawake wengine. Mwaka 1981 Mayaula Mayoni aliondoka Zaire akiwa na wanamuziki kutoka bendi ya Abeti Masikini waliohamia Afrika Magharibi ambako kati ya mwaka huo na 1984 alirekodi album kadhaa chini ya label ya Disc-Oriënt ya Lome, Togo.

Mwaka 1984 alirudi Zaire na mwaka 1986 alitoa album iliyoitwa Fiona Fiona, na mwaka huohuo Tshala Muana alipata umaarufu kutokana na wimbo Nasi Nabali, uliotungwa na Mayaula Mayoni.

Baada ya hapo akarekodi album yake ya Mizele akiwa na TP OK Jazz akisindikizwa na waimbaji Carlito Lassa na Malage de Lugendo. Mwaka 1993 alitoa album ya L'amour au kilo (yaani Mapenzi maziko kama kilogramu).

Albamu hiyo aliifanya akiwa na kundi la Soukous Stars lililowahusisha wanamuziki nyota kama Lokassa ya Mbongo, Ngouma Lokito, Balou Canta, Lucien Bokilo na wengineo.

Albam hiyo iliyokuwa na nyimbo nyingi kali kama Mbongo Ebima, ilifanya vizuri sokoni n ahata alipofanya ziara nchini Tanzania mwaka 1994 alipata mashabiki wengi licha ya kwanza wadhamini waliomleta walifanya ufisadi kiasi cha kushindwa kumlipa fedha zake, hivyo bendi hiyo kukwama jijini Dar es Salaam.

Wanamuziki wa bendi hiyo waliondoka kwa mafungu mafungu na Mayaula Mayoni, akiwa amempata mwanamke Mtanzania aliyekuwa akifanya kazi kwenye kampuni moja ya wakala wa utalii, akaamua kubaki kwa muda jijini humo. Miaka saba baadaye akatoa album nyingine ya Bikini.

Baada ya album hiyo Mayaula alihamia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi Ubalozi wa Congo. Hata hivyo, muda si mrefu akaanza kuugua na kuamua kurudi Matadi, kwao alikozaliwa.

Hali yake ilizidi kuwa mbaya mwaka 2005 akapelekwa Ubelgiji kwa matibabu na hatimaye kufariki dunia jijini Brussels Mei 26, 2010 akiwa na umri wa miaka 64. Alizikwa jijini Kinshasa. Mafanikio Katika maisha yake alichaguliwa mtunzi bora wa Zaire mwaka 1978 k









# Nje kwa kung'atwa na mbwa wake

**CANBERRA, Australia**

MLINDA mlango wa Sydney Sixers, Alyssa Healy, atakuwa nje ya Uwanja baada ya kujeruhiwa na mbwa wake.

Alyssa amesema alijeruhiwa mkono katika tukio la kutisha alipokuwa akiwatenganisha mbwa wake waliokuwa wanapigana nyumbani kwake.

Golikipa huyo alilazimika kufanyiwa upasuaji wa mkono hali iliyosababisha kukosa mechi ya Ligi ya Wanawake kati ya Big Bash dhidi ya Sydney Thunder.

Alyssa mwenye umri wa miaka 33 alisema aliweka mkono kati ya mbwa hao.

Hakupata uharibifu wa mfupa au mpasuko.

"Nadhani kulikuwa na mshipa uliohusika ambao pengine ulifanya ionekane zaidi kama tukio la uhalifu kuliko ilivyohitajika kuonekana Ilikuwa mbaya sana nilipotoa kidole changu hapo awali, nilifikiri nilikuwa kwenye ugomvi. Lakini yote yamekwenda sawa kwa sasa"Alisema.

Healy alichapisha picha yake akiwa na mkono uliofungwa kwenye mtandao wa kijamii , akisema anathamini "upendo wote" kutoka kwa wafuasi na alikuwa akitazama mchezo wao akiwa nyumbani.

Sixers wamesalia na mechi 12 za kundi na michezo yoyote inayowezekana katika hatua ya mtoano.

# Huyu Maddison ni suala la muda tu




**LONDON, Uingereza**

MASHABIKI wa Tottenham Hotspur wanafurahia maisha ya soka hivi sasa. Baada ya mechi tisa Tottenham wamefanya vizuri kufuatia mwanzo wao bora wa msimu tangu walipoweka rikodi kama hii mwaka 1960-61 .Msimu huu Tottenham walifanya usajili mazuri ambao unaanza kuonekana kuwalipa na kuwapa matokeo waliyokuwa wanayataka na kwa sasa ndio wanaoongoza katika msimamo wa ligi.

Utawala wa Ange Postecoglou kama mkufunzi wa Tottenham, baada ya kuwasili kutoka Celtic msimu wa joto, haukuanza vyema. Lakini baadae na mtindo wake wa kushambulia ulidhihirishwa na matokeo mazuri ikiwemo ushindi wa 2-0 wa Jumatatu dhidi ya Fulham.

Mabao kutoka kwa Son Heung-min na James Maddison yalihakikisha wanasalia moja kati ya timu mbili ambazo hazijafungwa kwenye ligi na, kwa sasa pointi mbili mbele ya kilele, wanatajwa hata kuwania taji.

Assists tano za Maddison kufikia sasa kampeni hii ni nyingi kuliko mchezaji mwingine yeyote kwenye Premier League, wakati Son ameongeza kasi bila ya Kane kufunga mabao saba moja tu ya mfungaji bora wa Premier League Erling Haaland.

Maddison alisema: "Tuna uhusiano mzuri. Sonny alikuwa mchezaji niliyempenda kwa miaka na miaka nikimtazama na sasa ni furaha kabisa kucheza naye."Yeye ni mchezaji wa kiwango cha kimataifa Siitupi hilo mara nyingi. Tunapenda kuungana, tunalifanyia kazi sana mazoezini na tunaanza kuelewana kuhusu mwenendo wa kila mmoja wetu."




# Afrika ipo kila kona

**NEW YORK,Marekani**

KILA msimu mpya wa NBA wasifu wa mpira wa kikapu wa Kiafrika unapanda juu.Hii inasababishwa na vijana mbali mbali wa kiafrica kufanya vizuri katika ligi hiyo.Ushiriki wa wachezaji kama Joel Embiid, ambaye msimu uliopita alikua nyota wa kwanza wa NBA mzaliwa wa Afrika kushinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Thamani (MVP) tangu Hakeem Olajuwon mnamo 1994.

Bingwa mara mbili wa NBA Olajuwon alizaliwa Nigeria lakini akachagua kuiwakilisha Marekani kama sehemu ya kile kilichoitwa "Dream Team" kwenye Michezo ya Olimpiki ya Atlanta 1996, uamuzi ambao Philadelphia 76ers katikati mwa Embiid waliuiga hivi majuzi, na kuwakatisha tamaa waliokuwa nchi yake ya kuzaliwa Cameroon

Kijana mwingine anayefanya vizuri ni Giannis Antetokounmpo, kutokea Nigeria ambaye alizaliwa Athens na anachezea Milwaukee Bucks, ni mmoja wa wachezaji waliopambwa sana katika historia ya shindano hilo, akishinda tuzo za MVP mfululizo mnamo 2019 na 2020, na kuiongoza Bucks kwenye ubingwa wao wa kwanza tangu 1971 mwaka uliofuata.

*HABARI HIZI ZIMEANDALIWA NA VALENSI MBAGA*

# El Hilal yaipiga chini TP Mazembe



El Hilal



Moise Katumbi

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa soka wa Sudan, El Hilal wamepiga chini ofa ya klabu ya TP Mazembe.

Mazembe walitoa ofa ya kuwapa El Hilal uwanja wao kwa ajili ya michuano ya Klabu Bingwa Afrika, kutokana na wasudan hao kukimbia machafuko nchini mwao.

Badala yake mabingwa hao wameamua kutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kama uwanja wa nyumbani.

Pamoja na Mazembe kutangaza ofa kwa El Hilal, timu hiyo inaweza pia kuhamia kwa Mkapa kutokana na msuguano ulipo Congo baina yao na serikali.

Upo uwezekano Mazembe walitaka kuitumia El Hilal kama kivuli cha wao kupewa kibali cha kuingiza vifaa vya kurushia matangazo ya michuano hiyo.

Katika mashindano yanayoendelea ya Ligi ya Afrika, Mazembe waulitumia Mkapa kutokana na sakata la matangazo ya televisheni.

Mabingwa hao wa Congo walipata mapokeo mazuri ya mashabiki kufurika hali iliyomfanya mmiliki wa timu hiyo, Moise Katumbi Chakwe kushuka jukwaani na kuzunguka uwanja mzima kuwashukuru watanzania.

## Manumbu atambulishwa Misri



**Na Mwandishi Wetu**

MCHEZAJI wa kimataifa wa Tanzania Suzan Manumbu ametambulishwa nchini Misri katika klabu yake mpya.

Suzan ambaye anacheza nafasi ya kiungo ametambulishwa katika klabu ya TUT FC inayoshiriki ligi kuu nchini Misri.

Kiungo huyo ametokea klabu ya Fountain Gate Princess ya Dodoma Tanzana na hatua hio inadhihirisha ukubwa wa ligi yetu na thamani yake katika mataifa mengine.

Suzan anaungana na wachezaji wengine wa Kitanzania ambao wanacheza ligi za wanawake kama wachezaji wa kulipwa.

Baadhi ya Wachezaji hao ni Juliet Singano anaekiwasha Juarez Feminin ya nchini Mexico, Aisha Mashaka anaekipiga pale BK Hacken ya nchini Sweden, Diana Lucas na Enekia Kasonga ambao wote wanacheza klabu ya Ausfaz ya nchini Morocco, Oppah Clement anaekiwasha Besikitas Vodafone ya nchini Uturuki, Mariam Yusufu anaekipiga PVP Buyenzi ya nchini Burundi , Fatuma mwisendi anaekiwasha pale Nees Atromitou WFC ya nchini Ugiriki.

Kutokana na kukua kwa soka la Tanzania imechangia hata soka kwa upande wa wanawake kukua na kugeuka kuwa ajira kwa wachezaji wetu wa ndani

## Katwila kama Roving DJ

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA,Zuberi Katwila ameanza rasmi kazi ya kukinoa kikosi cha timu ya Mtibwa ya Morogoro.

Katwila ambaye aliichezea Mtibwa kwa mafanikio mpaka alipostaafu soka, amejiunga na kikosi hicho baada ya kuondolewa Ihefu ya Mbarali, Mbeya. Kutokana na matokeo mabovu kikosini humo

Katwila aliondoka Ihefu siku chache baada ya Mtibwa kumpa mkono wa kwaheri kocha wao, Habib Kondo.


Kondo mchezaji wa zamani wa Simba na Sigara za Dar es Salaam aliondolewa Mtibwa kwa matokeo yasiyoridha akiifanya timu hiyo kutopata ushindi katika ligi kuu.

Katwila anarudi Mtibwa kama Kocha kwa mara ya pili .ambapo aliwahi kuifundisha mwaka 2014 hadi mwaka 2020/2021

Aliondoka hapo na kujiunga na Kagera Sugar ambayo pia ina undugu na Mtibwa sugar na alitumuliwa bada ya matokea mabovu na uchezaji mbovu wa timu



## Mchezaji mdogo zaidi AFL



**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI michuano ya Ligi ya Afrika (AFL) ikipamba moto, yapo mambo mazuri ambayo yanaonekana ,moja kati ya hayo ni uwepo wa vijana wadogo katika ligi hii na wakionekana kuaminika na timu zao na kuupiga mwingi.

Wapo wachezaji wengi wadogo ila Daniel Demegorgan Daga kutokea Enyimba Fc ndiye mchezaji mdogo zaidi,na akihudumu katika nafasi ya kiungo mkabaji wa timu hio.

Daniel ana umri wa miaka 16 na amekuwa pia akicheza timu ya Taifa ya vijana U20 na kufanikiwa kushiriki katika mashindano mbali mbali ikiwemo Kombe la dunia la vijana chini ya miaka 20 , na michuano ya kusaka tiketi ya Afcon 2023 chini ya miaka 20 iliyofanyika Senegal.

Daniel alikuwa kwenye kikosi kilichopambana wiki iliyopita dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco.Katika mchezo huo, Enyimba alipoteza kwa bao 1-0.

# Liverpool wataisumbua Man City

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Blackburn Rovers, Chris Sutton anaamini kuwa Liverpool watakuwa na changamoto kubwa kwenye ubingwa wa Ligi Kuu kwa Manchester City kuliko Arsenal. Mshambuliaji huyo anaamini kuwa nguvu ya Wekundu hao katika safu ya ushambuliaji itawasaidia kupanda dhidi ya vijana wa Pep Guardiola.

Hili limethibitika baada ya ushindi wao dhidi ya Everton kwenye mechi ya Jumamosi.

"Nadhani Liverpool itakuwa mpinzani mkubwa kwa Manchester City kuliko Arsenal, Mo salah amekuwa katika kiwango bora na kuwa moja kati ya watu muhimu katika kikosi hiko" alisema.

Beki wa zamani wa Manchester City, Micah Richards amemsifu Mohamed Salah kwa kufunga mabao mawili kwenye mechi hiyo, licha ya kuwa mechi mbaya zaidi ambayo amewahi kumuona akicheza.

Mmisri huyo alifunga mabao hayo dakika za mwisho na kupata ushindi dhidi ya Everton .




Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Oktoba 25 - 31, 2023 |


# Na badoo



**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa timu ya soka ya Yanga, Miguel Gamond amesema bado kikosi chake hakijafunguka.

Pamoja na kuwafunga Azam usiku mabao 3-2, Gamond amesema matokeo yalikuwa mazuri lakini anaamini Yanga inaweza kucheza vizuri zaidi ya pale.

"Unaangalia kiwango cha Aziz Ki, unamuangalia Max, unamuona Pacome naona pamoja na kucheza vizuri dhidi ya Azam lakini wanaweza kufunguka zaidi na tukapata mabao. mengi zaidi.

"Azam sio timu mbovu lakini tulisoma mchezo wao na kuangalia mechi zingine wanapocheza na pale wanapokabiliana na sisi, tukalazimika kwenda kivingine," alisema.

Kocha huyo alisema anafurahia matokeo ya ushindi ambayo pia yameonyesha ukubwa wa timu yake kama mabingwa watetezi.

Baada ya mechi ya juzi sasa Yanga itakuwa na kibarua kingine Ijumaa itakapokabiliana na Singida ambayo imeonekana kubadilika tangu ipate mwalimu mpya.

Singida ambayo haijawahi kupata matokeo kutoka kwa Yanga inataka kuendeleza furaha ya ushindi ambayo imeupata wiki iliyopita kutoka kwa Namungo na kumfanya Kocha Cedric Kaze kuachia ngazi

# El Hilal yaipiga chini TP Mazembe



Uk. 23

# Manumbu atambulishwa Klabu ya Misri

# Katwila kama Roving DJ



Uk. 23

# Wameumaliza Mwendo



**Na Mwandishi Wetu**

SAFARI ya wawakilishi wa Tanzania, timu ya Simba katika michuano Ligi ya Afrika (AFL) imeishia mjini Cairo, Misri.

Simba ilitoka sare ya bao 1-1 na mabingwa wa Afrika, Aly Hilal ya Misri.

Katika pambano la kwanza Simba walitoka sare ya mabao 2-2.

Simba ilicheza kwa kuzuia zaidi na kushambulia kwa kustukiza na kupata bao kupitia kwa Sadio Kanoute kabla ya Kahraba kuharibu ushindi ambao mnyama alitarajia kuupata.

Matokeo hayo yaliiweka Simba katika wakaru mgumu kutafuta nafasi ya kusonga mbele.

Sasa Ahly wanasubiri mshindi baina ya Mamelod Sundown na Petro Atletico ya Angola. Katika mechi ya kwanza, Mamelod waliishushia kipigo Atletico.

Sasa Tanzania itakuwa inaombea TP Mazembe ishinde mechi ya marudiano dhidi ya Esperance ya Tunisia ili watanzania waendelee kuona fainali hizo kwa Mkapa.